# KCSE 2026 FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## (MAJARIBIO YA UTABIRI 1-10)

**MWELEKEO WA MWISHO NA WA KIPEKEE KWA MAFANIKIO YA KCSE 2026!**

***Wape watahiniwa wako fursa bora zaidi ya ushindani kupitia mfululizo huu wa maswali ya utabiri yaliyofanyiwa utafiti wa kina. Toolkit hii madhubuti imeandaliwa kwa umakini mkubwa ili kuiga muundo na maudhui kamili ya mitihani ya mwisho ya KNEC, ikitoa mazoezi yenye tija ya juu na yanayolenga mtihani moja kwa moja. Hii ndiyo nyenzo thabiti na ya mwisho ya marudio ya kuongeza uelewa, kukuza hali ya kujiamini, na kuhakikisha alama za juu zaidi!***

***YAFUATAYO NI MASWALI YA KUTARAJIWA KATIKA MTIHANI WA KCSE 2026.***

## CONFIDENTIAL!

***Ukihitaji Mwongozo / majibu, Pigia***

***Bw. Isaboke 0746-222-000 / 0753-222-000***

# KCSE 2026 FINAL BLUEPRINT!

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 1

**102/1**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 1

**MUDA: SAA 1¾**

JINA……………………………………………………………………………………

SHULE…………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

1. *Andika Insha Mbili. Insha Ya Kwanza Ni Lazima.*
2. *Kisha Chagua Insha Nyingine Moja Kati Ya Hizo Tatu Zilizobaki.*
3. *Kila Insha Isipungue Maneno Mia Nne. 400*
4. *Kila Insha Ina Alama Ishirini. 20*
5. *Kila Insha Lazima Iandikwe Kwa Lugha Ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

**MASWALI**

**1. Lazima**

Kumekua na visa vingi vya utovu wa nidhamu shuleni. Wanakamati wa kitengo cha ushauri nasaha walijadiliana jinsi ya kuwahamasisha wanafunzi wenzao dhidi ya madhara ya utovu wa nidhamu katika maisha ya mwanafunzi. Wewe kama katibu wao, andika kumbukumbu za mkutano huo.

**2.** Wewe ni mkuu wa polisi katika Jimbo La Kazakamba. Andika hotuba utakayotoa kwa wanajamii wa Jimbo hilo kuhusu madhara ya ufisadi.

**3.** Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali; Chombo cha kuzama hakina usukani.

**4.** Tunga kisa kitakachomalizia kwa maneno haya; **...** kusema kweli sisi kama Wanajadi tulijutia mapuuza yetu katika shughuli ya uchaguzi uliokuwa umekamilika mwaka uliopita.

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 1

**102/2**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 2

**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………… SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO………………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

***Maagizo***

1. Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
3. Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | JUMLA | |

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Matumizi ya sheng' yameshamiri sana nchini Kenya hata rniongoni rnwa vijana. Ni kilugha ambacho kinakisiwa kuzuka katika miaka ya 60 na 70 katika makazi ya rnashariki mwa jiji la Nairobi kama vile Kaloleni, Mbotela, Bahati na kadhalika.

Kwa sasa ni kilugha kilichoenea kwingi nchini Kenya na kuwa kitambulisho cha takriban vijana wengi. Wataalam rnbalimbali wanabainisha nadharia mbalimbali kuhusu chanzo cha lugha hii. Kuna nadharia mbili kuu kuhusu asili ya lugha ya Sheng; kwamba kilugha hiki kiliibuka kutokana na wahuni na wakora jijini Nairobi ambao lengo lao lilikuwa kuwasiliana kwa siri. Nadharia nyingine ni kuwa kilichipuka kutokana na vijana ambao walizua lugha ya kuwasiliana baada ya uhuru kwa sababu walikichukia Kiswahili ambacho walikiona kama lugha ya uboi.

Dhana hizi kwa muda mrefu, zimeathiri mitazamo kuhusiana na kilugha hiki. Kwa sasa ni kilugha ambacho kinasambaa katika sehemu mbalimbali za Kenya na watu wa matabaka mbalimbali wanakitumia. Kilugha hiki kimeanza kuashiria uhalisia mkubwa wa maisha ya kisasa, zaidi katika jamii ya Wakenya. Aidha, sheng imejitanzua kutoka hali ye kuwa kilugha cha maongezi pekee na sasa kinatumiwa katika baadhi ya vitabu, hata waandishi wa vitabu wameanza kukitumia, kwa mfano katika miaka ya 80, David Mailu katika kitabu chake 'Without Kiinua Mgongo alitumia sheng.

Katika siku za hivi karibuni, Riwaya ya 'Kidagaa Kimemwozea' iliyoandikwa na Ken Walibora kilugha cha sheng kimepewa nafasi kama kitambulisho cha vijana kupitia kwa mhusika Di Bob.

Vilevile kumezuka vyombo vya habari kama redio, mfano idhaa ya Ghetto, redio ambayo inaendeleza mawasiliano kwa matumizi ya sheng. Kuna vipindi na matangazo ya kibiashara katika runinga ambayo yanaendelezwa kwa sheng. Kwa mfano katika gazeti a Taifa Leo, kuna ukumbi wa 'Mchongoano' ambao umekuwa ukiendelezwa kwa Sheng.

Nchini Kenya ambapo asilimia 60% ya idadi ni vijana, Sheng imetokea kuwatambulisha vijana. Katika enzi hii ya **Teknohama**, wanaomiliki vyombo vya habari na sekta nyingine za biashara wamegundua kuwa matumizi ya Sheng ndiyo njia mwafaka zaidi ya kulifikia soko kubwa la vijana kwa ajili ya kueneza matangazo ya bidhaa na huduma za kibiashara. Kwa hivyo, Sheng imekuwa daraja la kuwafikia na kuwavutia vijana.

Hata hivyo, kwa upande mwingine matumizi ya Sheng yamelaumiwa na walimu wengi katika shule za msingi na zile za upili kuwa ni sababu mojawapo kuu ya kushuka kwa matokeo ya lugha ya Kiswahili na Kiingeneza miongoni mwa wanafunzi. Sheng imelaumiwa kwamba inasababisha wanafunzi kutozingatia mafunzo ya kanuni za sarufi na tahajia au maendelezo. Wataalam wanadai kuwa ni **msimbo** ambao hauzingatii sheria za sarufi na tahajia kwa sababu zizizofahamika, kwani ingawa muundo wake wa kisarufi hushahabiana na ule wa Kiswahili, Sheng hupuuza sarufi ya Kiswahili katika matumizi yake.

Ingawa sheng imekuwa ikipigwa vita, kuna wataalam ambao wana mtazamo kwamba juhudi hizo haziwezi kufanikiwa kwani sheng ni chombo cha mawasiliano miongoni mwa vijana na kwa hivyo ma umunimu wake ambao hauwezi kufumbiwa macho. Wanasema kuwa ni chombo ambacho kinafumbata hisia na mshikamano wa kizazi kipya kama ilivyojitokeza katika kauli mbiu ye mgombeaji urais mwaka wa 2012,Tunawesmake.

Katika hali ambapo kiwango cha ubora wa matokeo ya Kiswahili yalidorora katika mtihani wa Kidato Cha nne (KCSE) mwaka wa 2012 na kuwa asilimia 35.81 pekee yakilinganishwa na asilimia 48.82 ya mwaka 2011, sheng imekuwa ikilaumiwa kuwa ndicho chanzo cha kudorora kwa viwango vya ubora wa matokeo. Baadhi ya hao wataalamu wanasema kwamba sheng haipaswi **kuhujumiwa**,kinachohitajika kufanywa ni kuwaelimisha vijana kuhusu mipaka ya matumizi yake.

**<u>Maswali</u>**

**(a) Taja** mada ya kifungu hiki. **(alama1)**

**(b) Fafanua** nadharia mbili zilizoeleza asili ya lugha ya Sheng. (**alama 2)**

**(c) Eleza** rnatumizi bainifu ya kilugha cha Sheng katika jamii ya sasa. **(alama 3)**

**(d) Taja** matokeo hasi ya matumizi ya Sheng katika jamii. **(alama 3)**

**(e) Ni** kwa nini mwandishi Walibora ameshirikisha matumizi ya Sheng katika kazi yake ya Kidagaa
Kimemwozea. **(alama 2)**

(1) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu hiki. **(alama 4)**

i) Teknohama

ii) Kudorora

iii) Msimbo

iv) Kuhujumiwa.

**2. UFUPISHO**

Kuna dhana nchini ambayo inazidi kuenezwa miongoni mwa vijana na usipochunga,tutakuja kujipata pabaya katika siku za usoni. Kwa kipindi cha miongo miwili hivi iliyopita, sekta ya sanaa nchini imekuwa ikiimarika kwa kasi. Kuna wasanii ambao wamefanikiwa kujiendeleza kimaisha kutokana na talanta zao lakini pia kuna wale ambao wamebaki katika hali ya uchochole, pengine kutokana na kuwa hawafahamu vyema jinsi ya kujisimamia na kutumia talanta zao kama mbinu ya kujipatia riziki. Kwa muda huo wote, vijana wengi wamejikuta wakivutiwa mno na hali ya kimaisha ya wasanhi waliobobea, hasa wanamuziki, na hivyo basi hujitosa kwenye sekta ya sanaa wakiwa na matumaini makubwa ya kuishi maisha ya kifahari.

Imefikia kiwango ambapo washikadau wa masuala ya kuendeleza maisha ya vijana, ikiwenio Wizara ya Michezo, Vijana na Utamaduni wanawekeza pakubwa kuendeleza sekta ya sanaa. Ni hapa ndipo wasiwasi unaibuka kwa kuwa huenda tukachukulia Kwamba juhudi za kuwezesha vijana kujikimu kimaisha
zitafanikiwa tu iwapo sekta ya sanaa itaimarishwa. Dhana hii ni potovu na ni sharti washikadau wazinduke, waanze kupanna mawazo yao na kuwa na busara kwenye hatua wanazochukua ikiwa wana nia ya kuwezesha vijana kujikimu kimaisha na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.

Ukichunguza kwa makini, utapata kuwa ni asilimia ndogo mno ya wanaojitosa kwenye sanaa ambao wanaweza kusemekana wana ari na kipawa cha kutosha kuweza, kuchangia ipasavyo kwenye uchumi wa kitaifa kwa kutumia vipawa hivyo. Hivyo basi, suala ibuka ni je, asilimia kubwa iliyosalia huwa wanafanya nini, na ni jinsi gani wanavyoweza kuwezeshwa wajiendeleza zaidi kimaisha? Hapatakuwa na haja ya kuwekeza mamilioni ya pesa katika kuendeleza sekta ambapo mapato yake hayatakuwa yenye faida kwa taifa.

Humu nchini tumekuwa na tabia ya kupuuza sekta zilizo muhimu sana, na matokeo yake ni kuwa tunaishia kuagiza bidhaa kutoka nje iihali tungeweza kujitengezea wenyewe nchini. Baadhi ya yale tuliyopuuza ni useremala, ushonaji wa nguo, utengezaji wa bidhaa za ngozi na hadi miaka ya hivi majuzi, kilimo kilikuwa kimezikwa kwenye kaburi Ia sahau miongoni mwa vUana. Ni kutokana na hali hii ambapo vijana wengi wanaochukua mikopo kutoka kwa hazina waliotengewa na Serikali huwa hawafanikiwi, kwa kuwa hakuna uwekezaji wa kutosha uliowekwa kuimarisha ujuzi wao wa kibiashara.

Kwa sasa, Serikali iko katika harakati za kuagiza vipakatalishi kutoka India. Na kumbuka vyema serikali ilivyotangaza kuwa vipakatalishi vitakuwa vikitengezwa nchini. Kwa kuviagiza kutoka mataifa ya kigeni, ni wazi kuwa hatujafikia kiwango cha kujitengezea vifaa hivyo kwa kiwango kikubwa, ingawa kuna watu kadha arnbao huagiza vipuri na kujitengezea kompyuta wenyewe. Vijana wanahitaji kuwezeshwa katika nyanja zote, na wala sb kwa sanaa na niichezo pekee.

Iwapo tutaendelea kutoa picha ya kuwa michezo na sanaa,pekee zilizo muhimu kwa vijana, itafika wakati ambapo tutaanza hata kuagiza mboga kutoka mataifa ya nje tusipojihadhari. Bila shaka tuna nafasi ya kurekebisha mienendo yetu, na ni vyema ikiwa tutachukua hatua hiyo haraka iwezekanavyo.

**Maswali**

(a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno 90-95. (alama 8,1 ya Utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Kwa kutumia maneno 70 - 75, eleza masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho (alama 5, 1 ya Utiririko.)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## <u>3. MATUMIZI YA LUGHA</u>

***a) Taja sauti mbili zenye sifa zifuatazo za matamshi.***

i) Mbele, wastani, tandazwa. **(alama 1)**

ii) Kati, chini, tandazwa **(alama 1)**

***b) Bainisha viambishi na mzizi katika neno kunipa. (alama 3)***

***c) Huku ukitoa mfano mmoja mmoja bainisha makundi matatu ya vivumishi vya sifa.*****(ala 3)**

***d) Huku ukipiga mstari, tunga sentensi moja yenye chagizo na yambwa.*** **(alama 2)**

***e) i) Kirai ni nini?*** **(alama 1)**

ii) ***Ainisha viral katika sentensi ifuatayo.***

Walimu hao hufunza wanafunzi kwa bidii. **(alama 2)**

***f) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale.***

Kitabu alichokinunua juzi kina uzuri niwingi. **(alama 4)**

***g) Huku ukitoa mfano mmoja mmoja, eleza namna tatu za kukanusha hali ya KU.*****(alama 3)**

***h) Andika wingi wa ukubwa wa sentensi ifuatayo.***

Huyu ndiye mwanamume mwembamba zaidi. (**alama 2)**

***i) Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi.***

Mwalimu alisema angemwadhibu rnwanatunzi siku illyofuata. **(alama 2)**

***j) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.***

Mtamba yule amekula nyasi nyingi. **(alama 1)**

***k) Kanusha sentensi ifuatayo kwa umoja.*** **(alama 1)**

Walipochekesha watu walipelekwa ng'ambo.

***I) Eleza maana tatu za sentensi ifuatayo.*** **(alama 3)**

Wakenya hawakienzi Kiswahili kama Watanzania.

***m) Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa nomino.*****(ala 2)**

Miachake **alilewa** hata akashindwa kutembea.

***n) Tumia neno makini kama kitenzi katika sentensi.*** **(alama 1)**

***o) Sahihisha sentensi ifuatayo.*** **(alama 2)**

Wasee hao waliwaambia wamama wale kuwa hawakuwa na kizazi nao hata baada ya kuwatusi vibaya.

***p) Tunga sentensi katika wingi ukitumia nomino hizi pamoja na kisisitizi mwafaka.*** **(al 2)**

i) noti

ii) kiziwi

***q) Tunga sentensi ukitumia nikama:***

i) Swali au kiulizi. **(alama 2)**

ii) Amri

***r) Tunga sentensi ukitumia neno labda kudhihirisha maana zifuatazo.*** **(alama 2)**

i) Shaka

ii) Uwezekano.

**4. ISIMU JAMII (AL.AMA 10)**

Utafiti wa kiisimu, Fasihi Simulizi na mapisi unaonyesha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kiafrika. Fafanua. **(alama 10)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 1

**102/3**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 3

**MUDA: SAA 2½**

**JINA…………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………………… SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI……………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO:**

**1)** *Jibu maswali **Manne** pekee.*
**2)** *Swali la **kwanza** ni la **Lazima**.*
**3)** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani; Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi, Riwaya na Ushairi.*
**4)** *Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu moja**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SWALI | MADA | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | TAMTHILIA | |
| 2 | RIWAYA | |
| 3 | HADITHI FUPI | |
| 4 | USHAIRI | |
| 5 | FASIHI SIMULIZI | |
| | JUMLA | |

**SWALI LA LAZIMA**

**SEHEMU A: RIWAYA**

**Clara Momanyi: Nguu za jadi**

**1. LAZIMA.**

"Dunia ni tambara bovu ... bovu sana. Ukivuta utachana. Acha waende zao."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. **(alama2)**

c) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(alama4)**

d) Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kutumia mifano kumi maridhawa riwayani. **(alama10)**

**SEHEMU B : TAMTHILIA**

**T.M Arege : Bembea ya Maisha**

**Jibu swali la 2 au la 3.**

**2.** Hayo ni ya kale ... na ya kale hayanuki. Wengi hawafuati tena mila hizo. Walimwengu sasa wanavaa sare moja.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

b) Fafanua tamathali mbili za usemi zilizotumika katika dondoo hili. **(alama2)**

c) Eleza sifa za mzungumzaji wa kauli hii. **(alama5)**

d) Jadili namna mila na tamaduni za Kiafrika zilivyomkandamiza mwanamke kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama9)**

**Au**

**3.** "Bila yeye chombo kingezama. Ni kwamba siwezi kumwambia haya maana atajishaua."

a) Kwa kutumia hoja tano, fafanua umuhimu wa mnenaji wa kauli hii katika kujenga tamthilia ya "Bembea ya Maisha" **(alama5)**

b) Fafanua madhara ya taasubi ya kiume katika jamii kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama7)**

c) Kwa kutumia hoja nane, tathmini ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kuzingatia mrejelewa na watu wa jinsia yake. **(alama8)**

**SEHEMU YA C: HADITHI FUPI**

**D.M Lutomia na P. Muthama (wah) : Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingine.**

**Jibu swali la 4 au la 5.**

**Dominic Maina Oigo: "Kifo Cha Suluhu."**

**4.** "Mume wangu, hebu zivute fikra zako miaka kumi na mitano iliyopita tulipoingia katika mkataba wa ndoa. Kwa nini unataka kujitia hamnazo kuhusu ahadi ulizozitoa? Umesahau namna tulivyohangaika, tukachekwa na watu, tukakosa hata marafiki na hatimaye tukabandikwa majina ya ajabu? Umesahau mume wangu? Umesahau namna kazi yako ya kuuza makaa ilivyofikia hatima ya ghafla baada ya serikali kupiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la Dafrau? Naomba ukumbuke. Ninaamini huenda umesahau! Ama cheo chako

cha ubunge ulichokipata kwa mbinu nizijuazo mimi kimekulevya na kukufanya uisahau familia yako?

a.(i) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama6)**

ii) Fafanua umuhimu wa ujumbe aliotoa mnenaji wa maneno haya kwa kutumia hoja saba. **(alama7)**

b) Kwa kutumia hoja saba, Jadili namna suala la dhuluma lilivyoshughulikiwa katika hadithi ya Sabina. **(alama7)**

Au

**NIPE NAFASI: MZAMANE NHLAPO**

5. "... Wanaume katika nyumba ile hawatulii. Walihisi kuwa mama alikuwa amewatusi na bila shaka kuna wale waliotamani wangekuwa na nafasi, wasingechelea kumtia mkononi na kumrudi vilivyo."

a(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

ii) Taja suala kuu linalojitokeza katika dondoo. **(alama1)**

iii) Fafanua umuhimu wa usimulizi katika hadithi hii. **(alama8)**

b) Kwa kurejelea hadithi "Toba ya Kalia" Jadili changamoto zinazokabili mayatima. **(alama7)**

**USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au la 7 .**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**.

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali
Ubavuni umuweke, umtowe kule mbali
Maskanini afike, umtindie fahali
Utamu anufaike, sima, bada au wali
Hatimaye ateuke, kwa viliwa vya samli
Mwanadamu simuamini, afadhali nyama lumbwi.

Mwanadamu umjenge, awe mwenye kutajika
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka
Nao mkono umuunge, vyake viwe vyaungika
Dhorubani umkinge, asipate kudhurika
Mara atakusahau, wema wako kafukia

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie
Amani yako umpeo, fanaka uirajue
Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue
Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue
Ndio wake mwelekeo, yuauma avuvie
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililo jema
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema
Viteko siwe akali, kumbizo zikaterema
Binadamu takudhili, dhili zako kazitema
Licha ya zote jamili, mwanadamu si muema
Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama

**Maswali**

a) Shairi hili ni la aina gani? Fafanua jibu lako. **(alama2)**

b) Eleza usaliti unaoendelezwa na mwanadamu kwa mjibu wa shairi hili. **(alama4)**

c) Tia shairi hili katika bahari tatu tofauti kwa kuzingatia; **(alama3)**

i) Mpangilio wa maneno

ii) Mpangilio wa vina

iii) Mgao wa mishororo

d) Eleza muundo wa shairi hili. **(alama4)**

e) Bainisha toni ya shairi hili. **(alama1)**

f) Eleza mbinu mbili ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa kwanza. **(alama2)**

g) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama4)**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini
Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
"Kuwa tayari kupanda na kushuka."

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka

Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendelee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijiokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla

**Maswali**

a) Fafanua mambo manne yanayokatisha tamaa katika shairi hili. **(alama4)**

b) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. **(alama4)**

i) Tashihisi

ii) Usambamba

iii) Mbinu rejeshi

iv) Tanakuzi

c) Fafanua aina tatu za taswira zilizotumika shairini. **(alama3)**

d) Onyesha aina tatu za urudiaji zinazojitokeza katika shairi hili. **(alama3)**

e) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. **(alama2)**

f) Tambua mifano miwili ya mistari mishata iliyotumika shairini. **(alama2)**

g) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. **(alama2)**

**8. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZE**

Mimi ni morani!
Nguli aliyekamilika
Nishatoka kumrarua simba dume
Kwa hii mikono miwili
Mimi ni shujaa asiyekanyaga kwa woga
Wala kubabaika
Simba mwenyewe ameungama
Mkuki wangu ni shahidi

Mimi ni jabali mtetemesha ardhi!
Azma yangu hairudi nyuma
Nguvu zangu hazimithiliki
Sina mzaha wala dhihaka
Mimi ni jasiri!
Ngao ndio hii hapa mkononi ni fumo nilirithi
Kujikinga na kulinda hadhi yangu
Yu wapi mwingine shujaa?

**Maswali**

a(i) Andika aina ya sifo hii. **(alama1)**

ii) Toa sababu nne kuthibitisha jibu lako la (i) hapo juu. **(alama4)**

iii) Tambua mbinu tano za lugha zilizotumiwa katika utungo huu. **(alama5)**

iv) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii nyingi. Fafanua kwa hoja tano sababu za hali hii. **(alama5)**

v) Kwa kutumia hoja tano, eleza njia zinazotumiwa na jamii ya kisasa kuendeleza kipera hiki. **(alama5)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 2

**102/1**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 1

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA**……………………………………………………………………………………

**SHULE**……………………………………………… **SAHIHI**………………………

**NAMBARI YA USAJILI**…………………………… **MKONDO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

a) *Andika jina lako na nambari ya usajili kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
d) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
e) *Kila insha isipungue maneno **400**.*
f) *Kila insha ina alama **20.***
g) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| **Jumla** | **40** | |

## MASWALI

**1. Lazima**

Wewe ni Mwalimu Mkuu katika Shule ya Upili ya Poromoka ambapo pamekuwa na visa vingi vya utovu wa maadili miongoni mwa wanafunzi. Waandikie wanafunzi wote memo ukiwaonya dhidi ya mambo haya.

**2.** "Utandaridhi una athari mbaya katika maisha yetu." Jadili.

**3.** Andika kisa kitakachoafikiana na methali: Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi.

**4.** Andika kisa kitakachomalizikia kwa: **...** walijifunga vibwebwe kuwavua wahasiriwa waliokuwa wamefunikwa na vifusi lakini jitihada zao ziliambulia patupu.

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 2

**102/2**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 2

**MUDA: SAA 2½**

**JINA…………………………………………………………………………………………**

**SHULE………………………………………………… SAHIHI……………………….**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………….. MKONDO……………………..**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

**(a)** *Andika jina lako na namba yako ya usajili shuleni katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**(b)** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**(c)** *Jibu maswali **yote.***

**(d)** *Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

**(e)** *Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. MUHTASARI | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMUJAMII | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

## 1. UFAHAMU

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Mbuga ya Ziwa Nakuru, sasa limesafishwa katika mojawapo ya juhudi za kukabiliana na maji taka yanayoingia mbugani. Wasimamizi wa mbuga walitumia huduma za vijana wasiokuwa na ajira kutoka mitaa ya Bondeni, Kivumbini, Lake view Freearea na Flamingo kusafisha mito inayobeba uchafu huo.

Vibarua walizoa jumla ya tani 1.5, na baadaye tani 4.2 idadi inayofikisha zaidi ya tani 6.0 kwa siku mbili mfululizo.Hili linaashiria jinsi kina cha uchafuzi wa mazingira kwenye ziwa Nakuru umeshamiri,na baadhi ya wafanyikazi wanaona litajwe kuwa janga la kitaifa linalokodolea macho mbuga nyingi humu nchini.

Shughuli hiyo ilivutia hisia mseto huku maswali mengi kuliko majibu yakiibuka, endapo KWS ina bajeti ya kung’arisha mbuga za wanyama.

Akizungumza na *Taifa Leo*, mwangalizi wa utalii kutoka kutoka mbuga ya wanyama ya Ziwa Nakuru Bw Sirman Kioko, alisema maji taka yamekuwa yakiingia kwenye mbuga kutokana na miundo msingi duni. Aliongezea kuwa maisha ya wanyama hasa simba, nyati, vifaru,nchui,nviboko na flamingo yalikuwa hatarini,kwa sababu ya maji taka yalikuwa yamebadili mkondo na kupenyeza kwenye mbuga.

Miaka mitano iliyopita mbuga ya Nakuru ilikuwa na idadi kubwa ya ndege aina ya heroe ,lakini sasa wamebakia 200 tu. Hali hii itazidi kuwa mbaya,endapo idara husika haitaweka mikakati ya kutafuta suluhu la kudumu kwa wanyama pori wanaozidi kuangamia. Aidha uchafuzi katika ziwa Nakuru umefanya ndege kuhamia ziwa Bogoria ambapo inaaminika angalau chakula ni tele.

“Tunakubali kuwa gharama ya kusafisha mbuga ni kubwa,lakini pia tunaomba umma kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki inayoziba njia za maji,”alisema.

Pia aliongezea kuwa ni jukumu la mbuga kusafisha mazingira ya wanyama,lakini baraza la mji wa Nakuru pia lina nafasi kubwa ya kuhakikisha makazi ya watu ni safi,kwa kuzoa taka ipasavyo. Anaona kuna utepetevu mkubwa kutoka kwa usimamizi wa mazingira NEMA,wanaostahili kuweka sheria kali za kukabiliana na wale wanaoharibu mazingira.

Aliongezea kuwa baraza la kusimamia huduma za wanyama pori (KWS),halina bajeti ya kusafisha mbuga na ndio sababu waliwaajiri vibarua saba kuendesha shughuli hiyo ya siku tatu. Uchafuzi wa mito inayoingia ziwa Nakuru hutokea msimu wa mvua ambapo maji hufurika na kusomba taka kutoka kwenye makazi ya watu.

Wanyama wanaovutia watalii kama vile Nyati hupata maradhi pindi wanapokunywa maji chafu,yaliyochanganyika na mifuko ya plastiki. Licha ya KWS kumiliki kituo cha kufanyia utafiti aina ya maradhi mbalimbali yanayokabili wanyama bado hawajafanikiwa kwa asilimia kubwa kuyazuia.

Hili linajiri siku moja tu baada ya wakazi wa mtaa wa Bondeni kuandamana barabarani wakilalamikia,ongezeko la kiwango cha takataka kwenye makazi ya watu.

**(Imenukuliwa kutoka kwa Gazeti la *Taifa Leo*)**

**Maswali**

**1.** Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. **(alama 1)**

**2.** Eleza sababu zinazofanya Ziwa Nakuru kuchafuka. **(alama 2)**

**3.** Ni nini madhara ya kuchafuliwa kwa Ziwa Nakuru? **(alama 4)**

**4.** Eleza vizingiti vinavyofanya ziwa hili kuendelea kuchafuliwa. **(alama 2)**

**5.** Toa mapendekezo yanayoweza kusaidia kumaliza uchafuzi wa Ziwa Nakuru kulingana na taarifa hii. **(alama 4)**

**6.** Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika taarifa. **(alama 2)**

**a.** Kupenyeza

**b.** Utepetevu

## 2. MUHTASARI

***Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu; kiumbe kilichopewa akili na maarifa fuvu tele ili kuratibu shughuli na mambo; kiumbe kilichopewa uwezo wa kuwasiliana na kutumia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala; kiumbe kilichopewa uwezo wa kufaidi viumbe wengine kwa njia mbalimbali na jumla jamala; hichi ndicho kiumbe kilichopewa idhini maalum ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama Hawa ambaye sasa amegeuka ndovu kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizonazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati zipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari; amefika mwezini; amevumbua mangala; amevumbua uyoka; amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni za kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.

Chambacho wavyele , akili nyingi huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole.

Rabana ndiye msanii asiye mfanowe kwani aliisawiri dunia kwa kila lililo jema kwa siku sita mtawalia na kumpa binadamu mazingira murua. Rabuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri ; akamwambia binadamu, ‘’Haya, twende kazi !’’

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji-taka ovyo hadi mitoni, maziwani na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambavyo ni urithi aliyopewa na muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili Maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sum na binadamu kwa sababu ya ‘maendeleo’ yake. Joshi kutoka katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozoni ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya asidi inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta mdhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa ‘tsunami’ bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na

kuwameza wazima wazima. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi. Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorokea wapi?

Idadi ya binadamu imezidi hadi kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza. Hii ni Imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe.

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengi kuangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemchemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia Kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya barafu.

**MASWALI**

**(a)**Jadili jinsi binadamu anaweza kutumia uwezo wake vizuri. **(alama 6)**

**Matayarisho**, **Jibu**

**(b**) Ukirejelea kifungu kizima, onyesha jinsi binadamu ametumia nafasi yake vibaya. **(alama 9)**

**matayarisho , Jibu**

**3. SARUFI**

**(a)** Linganua kwa namna mbili sauti /e/ na /a/ **(alama 2)**

**(b)**Andika neno lenye vipengele vinavyofuata vya kisarufi – kikanushi, ngeli, wakati,kitendwa, mzizi na kiishio. **(alama 2)**

**(c)** Tumia kitenzi kishirikishi kipungufu bila kupoteza maana ya sentensi hii. **(alama 2)**

Mwanafunzi mmoja angali analala bwenini

**(d)** Andika sentensi katika wakati usiodhihirika ukitumia nomino moja ya jamii. **(alama 2)**

**(e)** Tungia sentensi moja <u>ziara</u> na <u>maziara</u> ili kubainisha maana zao**.** **(alama 2)**

**(f)**Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. **(alama 2)**

Wanakujua huku.

**(g)** Sentensi zinazofuata ni za aina gani? **(alama 3)**

**(i)** Nyamari aliadhibiwa madhali alifika darasani akiwa amechelewa sana.

**(ii)** Mimi sijaelewa kamwe somo hili.

**(iii)** Watoto ambao walipotea juzi wamepatikana leo asubuhi

**(h)** Andika sentensi inayofuata katika usemi halisi ukianza na kihisishi cha dharau. **(alama 2)**

Mzee Anandwa alishangaa na kusema kuwa kijana huyo alikuwa amekuwa kaida kama Kirongwe.

**(i)**Bainisha tofauti na usawa kati ya mofimu na viambishi. **(alama 2)**

**(j)**Ainisha vishazi katika sentensi, **Endapo atanialika, nitamtembelea.** **(alama 2)**

**(k)** Tambua kiima, aina za shamirisho na chagizo katika sentensi hii. **(alama )**

Kimemletea taabu sana.

**Kiima: ……**

**Shamirisho: ….**

**Chagizo: ….**

**(l)** Andika umoja wa sentensi inayofuata katika hali yakinifu. **(alama 2)**

Kina mama wasingefika mapema fuoni, wasingewahi mashua.

**(m)** Tumia kivumishi cha a- unganifu katika sentensi ili kuleta dhana ya sifa. **(alama 2)**

**(n)** Tumia O rejeshi tamati**. Mwanafunzi ambaye hufanikiwa ni yule ambaye hudurusu kwa makini.** **(alama 2)**

**(o)** Bainisha matumizi ya **' KI'** katika sentensi hii. **(alama 2)**

Seremala akiwasili leo atakuwa akitengeneza kiti cha kitoto chake.

**(p)** Pambanua kwa michoro ya matawi sentensi inayofuata. **(alama 3)**

Ikiwa atawasili mapema, atafungua mkutano.

**(q)** Onyesha na ueleze matumizi ya viwakifishi vifuatavyo. **(alama 2)**

Kibainishi **…………………………………………………………………………………………**

Mkwaju **…………………………………………………………………………………**

**(r)** Tofautisha matumizi ya 'Ngali' katika tungo hizi. **(alama 2)**

Mama angali mlimani

Otiende angalisoma kwa bidi angaliishi maisha mema.

**(s)** Mkwezi hupanda miti **………………………………..** hufanya kazi maktabani, mpanzi **………………………..**, **……………………………** huendesha gari la moshi na mpagazi **(alama 2)**

**4. <u>ISIMUJAMII</u> (ALAMA 10)**

… Bwana Spika, ninaomba kufahamishwa kwa nini Waziri wa Biashara ameshindwa kuchukua hatua kukomesha uuzaji wa vileo hatari kwa watoto wa shule.

**(a)** Fafanua sifa zozote **tano** za sajili inayorejelewa na maneno haya. **(alama 5)**

(b) Eleza mambo yaliyochangia msambao wa Lugha ya Kiswahili kabla ya kuondoka kwa wakoloni barani. **(alama 5)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 2

**102/3**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 3

**MUDA: SAA 2½**

JINA…………………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Jibu maswali manne* ***pekee****.*

***b)*** *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima***

***c)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya Hadithi fupi,Tamthilia na Ushairi.*

***d)*** *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*

***e)*** *Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

**MBELE YA SAFARI**

**1.** Ilipoanza safari , ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

**2.** Njaa ikawa dhabiti ,na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti ,dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

**3.** Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari,utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari , juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

**4.** Ile ilikuwa ndoto , mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto,sahala 'mekuwa dhiki
Wagombanio kipato,utashi haukatiki
Nakutabakari

**5.** Msafara ukasita , kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita , mlima haupandiki
Basi sote 'kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

**6.** Tukiwa migongo wazi ,tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi , kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi ,Kuteremsha miliki
Wakaitapia

**7.** Wakafikia makazi,ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

**8.** Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema , kwa umati halaiki
Imezima nia yote ,kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

**a)** Eleza safari inayolejelewa katika shairi hili. **(al 2)**

**b)** Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. **(al 6)**

**c)** Taja na ueleze bahari mbili za shairi ukizingatia : **(al 4)**

- **i.** Mizani
- **ii.** Vina

**d)** Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. **(al 4)**

**e)** Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita **(al 4)**

**f)** Eleza umbo/ muundo wa shairi hili. **(ala 2)**

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**

**Timothy Arege;BEMBEA YA MAISHA**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. (a.) Soma dondoo lifuatalo kasha ujibu maswali.

**Sara :** Mimi ninashukuru kwa hawa alionipa mungu. Nikitaka zaidi nitakuwa mchache wa shukrani.(kimya) Dina nimesemwa sanana kutukanwa kwa sababu ya hawa wasichana wangu. Wewe unajua yote yaliyosemwa, hadharani na faraghani. Si makanisani, si magengeni. Leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao, ninaridhika moyoni. Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika. (Anatokwa na machozi)

Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha.

i.) Changanua maudhui katika dondoo hili **(ala 3)**

ii.) Bainisha toni katika dondoo hili **(ala 2)**

iii.) Tambua mbinu tatu za lugha ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. **(ala 3)**

(b.) Jadili jinsi suala la utu linavyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea Ya Maisha**(ala 12).**

**AU.**

**3**. Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(ala 20)**

**SEHEMU YA C: RIWAYA** C. MOMANYI: **NGUU ZA JADI**

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."

(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**

(b) Anayesema maneno haya ni jasiri. Thibitisha kwa hoja tano. **(alama 5)**

(c) Tathmini kwa hoja kumi na moja nafasi ya wenye pesa katika kuendeleza tamaa na ubinafsi katika nchi ya Matuo. **(alama 11)**

**AU**

**5.** "Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu?" alijiskia kusema. Alishusha pumzi kwa nguvu akajiuliza kimoyomoyo kwa nini Mungu aliruhusu moto kumtia kwenye shimo la maangamizi na wanawe. Hata hivyo, aliamini kuwa wakati mwingine Mungu huruhusu mabaya kutokea ili kuwafunza waja. Waaidha, alijua kuwa mashaka yanapomkumba mja, huwa ni funzo pia. Humtayarisha kuyahimili machungu zaidi ulimwenguni ama kumuasa dhidi ya kuabudu maovu. Maovu yanapotendwa na wachache, hata wale wasio na hatia pia hujikuta wamo humo uovuni. Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.

**(a)** Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 5)**

**(b)** Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisani aliko Mangwasha katika kukuza Riwaya ya Nguu za Jadi **(alama 5)**

**(c)**Nchi ya matuo imeshinikizwa na Nguu Za Jadi zinazorudisha nyuma usawa katika jamii. Tathmini kauli hii kwa hoja kumi. **(alama 10)**

## SEHEMU YA D :HADITHI FUPI

***MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE***

*Jibu swali la 6 au 7*

**WINNIE NYARURI OGENCHE: ''SABINA''**

**6.** ''Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.''

**a)** Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika.** **(alama 6)**

**b)** Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. **(alama 4)**

**c)** Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. **(alama 10)**

**YUSSUF SHOKA HAMAD: ''*Mzimu wa Kipwerere*''**

**7.“…**Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama.”

(a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(Alama 4)**

(b)Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(Alama 4)**

(c)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. **(Alama 2)**

(d)Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. **(alama 10)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***Swali la nane***

**8. a)** Ulumbi ni nini**?** **(alama 2)**

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii?. **(alama 6)**

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi**.** **(alama 6)**

**b)** Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. **(alama 6)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 3

**102/1**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 1

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA**……………………………………………………………………………………

**SHULE**…………………………………………… **SAHIHI**………………………

**NAMBARI YA USAJILI**…………………………… **MKONDO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**(INSHA)**

**Maagizo**

*(a)* *Andika insha* ***mbili****.*

*(b)* *Insha ya kwanza ni ya* ***lazima*** *kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia*

*(c)* *Kila insha isipungue maneno* ***400***

*(d)* *Kila insha ni alama 20*

*(e)* *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**MASWALI.**

**1. SWALI LA KWANZA**

Unataka kuanzisha shule ya kibinafsi (kiwango cha sekondari) mwakani.Andika tangazo litakalovutia wazazi na wanafunzi watakaoleta watoto wao au watakaojiunga na shule yako.

**2.** Teknolojia ya kisasa ni kama sarafa yenye sura mbili.faida na madhara. Jadili.

**3.** Usipoziba ufa utajenga ukuta.

**4.** Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya **……..**ilinichukua muda mrefu kuyaamini niliyoyasikia.

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 3

**102/2**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 2

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………… SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha na Isimu Jamii)**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

*Jibu maswali yote.*

*Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

*Karatasi hii ina kurasa nane. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |
| | | |

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Ni dhahiri shairi kwamba uharamia umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za karibuni.Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika mashariki.Taarifa za Uharamia zimetawala vyombo vya habari. Kiasa cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani.Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kutiwa kwenye mizani.

Yamkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwana kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mijini Nairobi na Dar es Salaam mnamo Agosti 7.1998 na tukio la septemba 11, mwaka 2001 kule marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la maana kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao.Kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala wajibika katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelenga jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umaskini na magonjwa yaliyoshesheni pakubwa barani.Bila shaka, hili ni suala linalilozalishwa kinyume mbele. Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa,kunaelekea kuzipiga jeki juhudi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, inayochangia upungufu na ucheleweshi wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi.Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya milenia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikikiano wa maendeleo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Ni muhali kwa utalii kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama, ikakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitahidi za kuweka laini mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtandao ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kutafutia juhudi za maharamia katika bahari Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni.Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyenginezo kwenye kanda ya mwambao zimetiliwa shaka si haba. Itabidi mikakati na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

## MASWALI

**a)** Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni? **(alama 3)**

**b)** Fafanua dhana ya "kinyume-mbele" kwa mujibu wa taarifa hii. **(alama 2)**

**c)** Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi.fafanua. **(alama 3)**

**d)** Thibitisha kwa kuwa Kenya imeathirika pakubwa kutokana na vitendo vya uharamia.

**(alam4)**

**e)** Ukirejelea kifungu, eleza maana ya **(alama 3)**

**i)** Uharamia

Mtandao

**ii)** Mwambao

## 2. UFUPISHO Alama 15

***Soma kifungu hiki kisha ukifupishe kwa kujibu maswali yatakayofuata.***

Ukitaka kufaulu maishani lazima ujue kuwa una kazi kubwa sana inayokungoja. Baada ya kuikabili vilivyo kazi hiyo kwa kutumia Nyanja mbalimbali utayaimarisha maisha yako. Karibu kila mtu aliyestawi amepitia katika vikwazo vingi tena vya kutatiza kuliko vikwazo wanavyovipata vijana wa kisasa. Vijana wote wanatakiwa sasa wasugue bongo zao sawasawa watende mambo mengi mazuri kuliko yale wanayoyaona. Wasitosheke na yale yaliyotendwa na wazee. Kila kijana iwapo atakuwa na moyo kama huo nchi zote zitaendelea kwa kasi.

Kwa kujisaidia katika kujiendeleza, yafuatayo yanafaa kuzingatiwa.Vijana wanatakiwa wawe watoto wenye kuelewana na wazazi wao ambao watawaelekeza vyema kitabia na wakiwa ni wazazi waelewa, watapata watoto wao maelekeo na radhi ambayo ni bora kuliko mali.watoto wenyewe wajue wanataka nini, wawe na malengo katika maisha yao na wakazanie kupata kile wanachokitaka bila kukata tamaa,watie bidii sana, wapende kusoma bila kulazimishwa kwani kulazimishwa hakusaidii chochote. Ni sawa na ng'ombe alazimishwaye kwenda kunywa maji lakini akifika mtoni akatae kunywa maji yale.Mtoto mwenyewe anatakiwa ajitafutie na ajue kuwa hasara ni yake asipofanya bidii na ajiamshe kifikira.Mtoto huyu asiridhishwe na vitu vidogo vidogo ama kuwa wa tamaa anayependa kupewa zawadi ama peremende kila saa. Lazima ajue kuwa kupewa au kutopewa ni mamoja.Wazazi wakiwa na kitu cha kumpa ni sawa, wakiwa hawana pia sawa.Mtoto anatikiwa kuwa muelewa sana.Anatakiwa awe na ile fikira ya kujitafutia. Hata kama anatoka katika hali ya utajiri azidi kutafuta ili ikiwezekana atajirike hata Zaidi.Asitegemee cha ndugu kwani huenda akafa akiwa maskini. Chako ni bora kuliko kikubwa cha mwenzio.

Vijana wanatakiwa kuwa na nidhamu ya kiwango cha juu popote walipo. Wawe ni watu wenye kujiamini. Wasikate tamaa kwa ajili masomo ni magumu bali wakazane kuyaelewa kwani mwisho, wataelewa na kufanikiwa.Yafaa waelewa kuwa hakuna kizuri kinachopatikana kwa urahisi, mtaka cha mvunguni sharti ainame. Lazima wadhurike wakitaka kufarikiwa.

Wasiwadharau walimu au wenzao, wasipoteze wakati wao kusengenya. Wawapuuze wanaowanyanyasa,hata neno moja la kuwaudhi wanaloambiwa na watoto waovu. Vijana wawe tayari kukosolewa na kuomba msamaha wa makosa yao. Wewe ni watu wanaowaelewa wenzao na kuwachukulia vizuri, wawaheshimu kwa vile walivyo.Wasithamini vitu vya anasa sana kama mavazi ya kitajiri wengi wasio na chochote wanaopuuza mambo ya anasa ndio wanaofaulu sana katika maisha. Wenye tamaa hawafaulu, hugeuka kuwa wezi na kuishia gerezani.

**MASWALI**

**a)** Fupisha aya ya kwanza kwa maneno 30. **(alama 5** mtiririko 1)

**b)** Bila kupotosha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi, fupisha aya mbili za mwisho. (maneno 95-100) **(alama 10** mtiririko, 2)

**3.LUGHA** **(Alama 40)**

**a)** Taja sauti mbili zinazotamkiwa kwenye kaakaa laini **(alama 1)**

**b)** Eleza tofauti za sentensi zifuatazo **(alama 2)**

i) Amerudi shuleni!

ii) Amerudi shuleni.

**c)** Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mstari.

i) Afisa mkuu anafuata sheria <u>sembuse</u> wewe. **(alama 1)**

ii) Ameenda huko mbali <u>sokoni</u> **(alama 1)**

**d)** Tambua aina ya vihusishi katika sentensi zifuatazo

i) Jumba alifuatalo li mbele ya msikiti wa Musa **(alama 1)**

ii) Kisiwa cha Ginigi kimekauka **(alama 1)**

**e)** Tambua hali katika sentensi ifuatayo.

Vyungu vya aina hii vyafinyangwa na huyu. **(alama 1)**

**f)** Toa maana mbili za neno lifuatalo **(alama 2)**

Somo

**g)** Kanusha

Mama alimwambia sipo alime haraka **(alama 1)**

**h)** Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano

**i)** Lia (Kutendeshwa) **(alama 1)**

**ii)** -Ja (Kutendea) **(alama 1)**

**i)** Andika katika hali ya wastani umoja

Kigombe kile kiliumia kikwato **( alama 2)**

**j)** Akifisha sentensi ifuatayo.

Je kuna manusura wowote yeye alitaka kujua. **(alama 2)**

**k)**

**i)** Eleza maana ya kirai **(alama 1)**

ii) Onyesha aina ya virai katika sentensi ifuatayo.

Nilimpata akilalama ndani ya darasa **(alama 2)**

**l)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.

Mwelekezi wake alimwambia kuwa angeweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa angeyafuata mashauri yake. **(alama 2)**

**m)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale.

Mtoto mmoja aliyekuwa mgonjwa sana alitibiwa jana. **(alama 4)**

**n)** Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia "o" rejeshi

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo **(alama 1)**

**o)** Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo

Wachimba migodi wanafanya kazi haraka ipasavyo. **(alama 2)**

**p)** Tumia kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi katika sentensi **(alama 2)**

**q)** Onyesha viambishi katika fungutenzi hili **( alama 2)**

**Sajilika**

**r)** Eleza matumizi ya "na" katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Ndovu aliuawa <u>na</u> wawindaji haramu <u>na</u>mi nikawaripoti

**s)** Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo **( alama 2)**

i) Takrimu

ii) Sakini

**t)** Weka vitenzi hivi katika hali ya kuamrisha kulingana na maelezo katika mabano **(alama 2)**

i) -nywa (umoja)

ii) Tubu (wingi)

**u)** Weka neno lifuatalo katika ngeli mwafaka **(alama 1)**

**Nyasi**

## <u>ISIMU –JAMII</u>

**4. a)** Eleza mitazamo mitatu kuhusu chimbuko la Kiswahili **(alama 6)**

b) Taja sifa nne za sajili ya utingo

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 3

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA**……………………………………………………………………………………

**SHULE**…………………………………………… **SAHIHI**………………………

**NAMBARI YA USAJILI**…………………………… **MKONDO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**Fasihi**

**MAAGIZO**

- *Jibu maswali **manne** pekee.*
- *Swali la **kwanza** ni la **lazima.***
- *Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemunne zilizobaki – yaani Riwaya, Tamthilia, Ushairi na FasihiSimulizi..*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- *Kila Swali lina alama**20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | |

**SEHEMU A:**

**FASIHI SIMULIZI**

**LAZIMA**

1. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Mimi ni Olichilamgwara
Olichilamgwara mwana mbee wa Ojilong
Ojilong wa Marukatipe
Wazee waliposhindwa
Nilivuka misitu milima na mito
Ni mimi jabali
Kipande cha jifya la mama
Nilipokuwa nalisha mifugo
Nilisikia baragumu inalia
Baragumu ya wito
Mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Nikachukua mkuki wangu
Wenye kigumba cha mti
Nikachukua upanga wangu
Wenye makali kama mmweso wa radi
Upanga uliopasua pembe za nyati kwa dhoruba moja
Ndipo nilipofyatuka kasi kama umeme
Kufumba kufumbua nikawakaribia nduli
Kusikia vishindi vyangu wakaanza kubabaika
Kuona kifua changu cha manyoya ya kanga wakatetemeka
Macho yangu makali kama kaa la moto yalipowatazama wakakimbia
Mkuki wangu ulipaa kama umeme
Wote wakalala
Mifugo wakanifuata…
Mko wapi vijana
Mmekuwa kama majivu baada ya moto kuzimika?

**Maswali**

a) Tambua kipera ulichokisoma na udhibitishe jibu lako **(al. 2)**
b) Tambua sifa za jamii zinazosawiriwa katika utungo huu **(al. 2)**
c) Kwa kutoa mifano bainisha vipengele vine vya kimtindo vilivyotumiwa na nafsineni **al. 4)**
d) Fafanua sifa nne za kipera hiki **(al. 4)**
e) Eleza mambo manne ambayo mtendaji wa kipera hiki anaweza kufanya ili kufanikisha utendaji wake. **(al. 4)**
f) Fafanua mikakati ambayo jamii inaweza kutumia ili kuzuia tungo kama hizi kufifia **(al. 4)**

**SEHEMU YA B: USHAIRI**

**Jibu swali la 2 au 3**

**2. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wao ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurai Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanunua mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu', kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza vunja kaniyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Ninacho change killo, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadi ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**MASWALI:**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. **(alama 1)**
b) Fafanua mambo **matatu** ambayo nafsineni analalamikia. **(alama 3)**
c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. **(alama 3)**
   (i) Idadi ya vipande katika kila mshororo
   (ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti
   (iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti
d) Andika ubeti **wa nne** katika lugha nathari. **(alama 4)**
e) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. **(alama 2)**

g) Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

h) Fafanua muundo wa ubeti **wa tano**. **(alama 3)**

**3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tilichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisa kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hiii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa.
Iwapo wewe ni mme,

Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha **(al. 2)**

b) Tambua anayeimba na anayeimbiwa shairi hili **(al. 2)**

c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume **(al. 2)**

d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili **(al. 4)**

e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili **(al. 2)**

f) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiuarudhi **(al. 4)**

g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? **(al. 4)**

i) Mbari
ii) Msununu
iii) Ngariba
iv) Uvundo

**SEHEMU C: TAMTHILIA; BEMBEA YA MAISHA – TIMOTHY M. AREGE**

**Jibu Swali la 4 au 5.**

4. **"Huku ndiko kuvumilia hasa. Tazama faraja ilivyoalika sasa"**

a) Weka dondoo hili katika muktadha. **(alama 4)**

b) Eleza sifa za msemaji katika dondoo. **(alama 6)**

c) Onyesha jinsi faraja ilivyoalika katika maisha ya msemewa kwa kurejelea tamthilia ya: Bembea ya Maisha. **(alama 10)**

**AU**

**5.**

**(a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho.** **(alama 10)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (*Kimya*). Siku hazigandiwala jana hairudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (*Kimya*). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (*Kimya*). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya

zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! *(kama anayeisemea pombe).* Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. *(anapunga mkono.)* Kwaheri pombe. Buriani.

b) Bainisha toni ya dondoo hili. **(alama 2)**
c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima**.(alama 8)**

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**Jibu swali la 6 au 7**

**6. Harubu ya maisha *Paul Nganga Mutua***

"Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…"
(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake **(al. 4)**
(b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii **(al. 6)**
(c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii **(al. 10)**

**7. D.W .LUTOMIA : *Msiba wa kujitakia***

**Wetu ni wetu ,hata akiwa mbaya …ni wetu.hatuna budi kuchagua yeye .lisilobudi hubidi.**
(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4)**
(b)Fafanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hii. (**alama 4**)
(c)Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai.jadili.(**alama 12**)

**SEHEMU YA E: RIWAYA- NGUU ZA JADI**

8. Hivyo,alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa samba. <u>Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi.</u> Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasisi hao?.

(a) Eleza mbinu nne za mimtindozinazojitokeza katika dondoo **(al 4)**
(b) Eleza sababu za msemaji kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari **(al 10)**
(c) Eleza umuhimu wa msemaji katika kujenga ploti ya riwaya hii **(al 6)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 4

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

JINA………………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

*(a) Andika insha **mbili**.*
*(b) Insha ya kwanza ni ya **lazima** kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia*
*(c) Kila insha isipungue maneno **400***
*(d) Kila insha ni alama 20*
*(e) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

## Lazima

**1**. Siku za hivi karibuni umesoma riwaya mpya iliyoandikwa na Msanifu Kombo inayoitwa : Afrika imelaaniwa. Andika tahakiki ya riwaya hii.

**2.**Hatua ya serikali kuu kumpa kila mwanafunzi wa darasa la kwanza tarakilishi ni manufaa sana. Jadili

**3**.Andika kisa kitakachodihirisha ukweli wa methali ifuatayo:

Ukiona cha mwenzako kikinyolewa na chako tia maji

**4.**Andika insha itakayomalizikia kwa kauli hii: Ama kweli sikufikiria wala kutegemea kuwa aushi yangu ingebadilika jinsi hiyo.

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 4

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA…………………………………………………………………………………………**

**SHULE………………………………………………… SAHIHI………………………..**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………….. MKONDO…………………….**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

*Jibu maswali yote.*

*Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

*Karatasi hii ina kurasa nane. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |
| | | |

## 1.UFAHAMU (Alama 15)

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake mkuu.

Yeye hutarajia kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia watoto na daima dawamu kuwa **'mwendani wa jikoni'** akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. Akanyagapo **mume naye papo huutia wayo wake.**

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, Historia, Jiografia, Hesabu, Sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya. Akataka kuwa mwalimu, akawa.Akataka kuwa daktari, akafanikiwa.Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa **hateswi akafyata ulimi.** Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali 'mahali pake' katika jamii alipotengewa na wanaume wenye **mawazo ya kihafidhina** yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha **ukatani.**

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo, lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanamume wa 'kisasa', ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama mshiriki sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya **aushi.**

## Maswali

**a)** i) Msemo 'mwendani wa jikoni' unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii?**(al1)**

ii) Thibitisha hali uliyotaja hapo juu kwa kutoa hoja nne. **(alama 2)**

**b)** Mwandishi ana maana gani anaposema 'akanyagapo mume naye papo huutia wayo wake'

**(alama 1)**

**c)** Tofautisha mwanamke wa kiasili na wa kisasa ukizingatia maswala ya ndoa na elimu. **(alama 4)**

**d)** Eleza hoja sita zinazoonyesha kuwa wanaume wana 'mawazo ya kihafidhina' dhidi ya mwanamke. **(alama3)**

**e)** Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. **(alama2)**

**f)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. **(alama 2)**

i. Ukatani

**ii.** Aushi

## 2. UFUPISHO (ALAMA 15)

***<u>Soma kifungu kifauatacho kisha ujibu maswali.</u>***

Mifuko ni muhimu sana katika maisha ya binadamu ya kila siku. Baadhi ya mifuko huundwa kwa namna ambayo inadumu na inaweza kutumiwa mara kadha wa kadha. Hii huweza kuhifadhiwa na kutumiwa kwa kipindi kirefu. Asilimia kubwa ya mifuko ya aina hii hutengenezwa kutokana na nguo au ngozi. Hata hivyo, ipo mifuko mingine ambayo si ya uashi, haidumu. Hii ni mifuko myepesi, rahisi kubebeka na inayopatikana kwa wingi sana. Hii ni mifuko ya plastiki.

Mifuko ya plastiki hupatikana katika maeneo mengi sana. Mifuko hii sio ghali inapolinganishwa na ile ya nguo au ya ngozi. Hii ni ya gharama ya chni na hupendwa kutokana na wepesi wake. Hata hivyo, mifuko hii inaweza kuwa chanzo cha matatizo mengi. Matatizo haya hutokana na linalopasa kufanywa kuhusu mifuko hii baada ya kutumiwa kwake. Mifuko ya nguo ambayo inatupwa kwenye jalala huishia kuoza na kuwa sehemu ya uchafu wa jalala hilo. Kwa upande wake, mifuko huo. Hata inapofukiwa arthini haiwezi kuoza hata kama kufukiwa huko ni kwa miaka mingi. Aidha hata pale inapochomwa, haiwezi kuteketea hadi kuwa jivu kama ilivyomifuko ya karatasi.

Upo umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa sera madhaubuti za kupambana na tatizo la mifuko hii. lazima zitungwe sheria ambazo zinakabiliana na uchafuzi wa mazingira kwa njia hii. kwa njia hii hatari zianzowakabili watu na wanyama zitapunguzwa kwa kiasi kikubwa. Kwa hakika njia mojawapo ambayo ingeweza kutumiwa ni kuharamisha matumizi ya mifuko hii katika upakiaji. Sheria zinaweza kupitishwa ambazo zinahimiza matumizi ya mifuko mbadala kama ile ya karatasi kubebea vitu vidogo Fauka ya hayo, pana haja ya kuwazia kuwepo kwa njia nzuri kuteketezea mifuko hiyo. Inawezekana kuhimiza watumiaji kuirejesha mifuko hiyo mahali Fulani kwa ajili ya uteketezaji huo. Hata hivyo, hali hii huenda ikawa ngumu kwa kuwa inahitaji nidhamu ya hali ya juu sana kwa upand ewa watumiaji.

**(a)** Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 105 – 110. **(alama10,1 utiririko)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza katika aya ya mwisho **(maneno 50 – 55) (alama 5, 1 utiririko)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## 3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

**a)** Taja sauti mbili zinazotamkiwa kwenye kaakaa laini **(alama 1)**

**b)** Eleza tofauti za sentensi zifuatazo **(alama 2)**

i) Amerudi shuleni!

ii) Amerudi shuleni.

**c)** Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mstari.

**i)** Afisa mkuu anafuata sharia <u>sembuse</u> wewe. **(alama 1)**

**ii)** Ameenda huko mbali <u>sokoni</u> **(alama 1)**

**d)** Tambua aina ya vihusishi katika sentensi zifuatazo

i) Jumba alifuatalo li mbele ya msikiti wa Musa (alama 1)

ii) Kisiwa cha Ginigi kimekauka **(alama 1)**

**e)** Tambua hali katika sentensi ifuatayo.

Vyungu vya aina hii vyafinyangwa na huyu. **(alama 1)**

**f)** Toa maana mbili za neno lifuatalo **(alama 2)**

Somo

**g)** Kanusha

Mama alimwambia sipo alime haraka **(alama 1)**

Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano

**i)** Lia (Kutendeshwa) **(alama 1)**

ii) -Ja (Kutendea) **(alama 1)**

**h)** Andika katika hali ya wastani umoja

Kigombe kile kiliumia kikwato **(alama 2)**

**i)** Akifisha sentensi ifuatayo.

Je kuna manusura wowote yeye alitaka kujua. **(alama 2)**

**i)** Eleza maana ya kirai **(alama 1)**

ii) Onyesha aina ya virai katika sentensi ifuatayo.

Nilimpata akilalama ndani ya darasa **(alama 2)**

**j)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.

Mwelekezi wake alimwambia kuwa angeweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa angeyafuata mashauri yake. **(alama 2)**

…………………………………………………………………………………………………

**k)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale.

Mtoto mmoja aliyekuwa mgonjwa sana alitibiwa jana. **(alama 4)**

**l)** Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia "o" rejeshi
Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo **(alama 1)**

**m)** Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo
Wachimba migodi wanafanya kazi haraka ipasavyo. **(alama 2)**

**n)** Tumia kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi katika sentensi **(alama 2)**

**o)** Onyesha viambishi katika fungutenzi hili **( alama 2)**
Sajilika

**p)** Eleza matumizi ya "na" katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**
Ndovu aliuawa <u>na</u> wawindaji haramu <u>na</u>mi nikawaripoti

**q)** Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo ( alama 2)
i) Takrimu
ii) Sakini

**r)** Weka vitenzi hivi katika hali ya kuamrisha kulingana na maelezo katika mabano **(alama 2)**
i) -nywa (umoja)
Tubu (wingi)

**s)** Weka neno lifuatalo katika ngeli mwafaka **(alama 1)**
Nyasi

**4. <u>ISIMU JAMII (ALAMAMA 10)</u>**

Eleza sababu za vijana kutumia lugha ya sheng' **(alama 10)**

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 4

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

JINA………………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI……………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
- *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima.***
- *Maswali hayo mengine* ***matatu*** *yachaguliwe kutoka sehemunne zilizobaki – yaani Riwaya, Tamthilia, Ushairi na FasihiSimulizi..*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- *Kila Swali lina alama**20***

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | |

1) **SEHEMU YA A- LAZIMA**

**RIWAYA YA NGUU ZA JADI NA PROFESA CLARA MOMANYI**

"Samahani… Nina shida kidogo. Ninaomba usaidizi. Sikuwa nikilipa ushuru katika biashara zangu. Sasa wanataka kuzifunga na kunipeleka kotini."

a) Eleza muktadha wa dondoo **(alama 4)**

**b)** Bainisha toni katika dondoo hili **(alama 2)**

c) Eleza sifa nne za msemewa **(alama 4)**

**d)** Msemaji wa maneno haya na wengine ni adui ya wananchi wa Matuo. Eleza ukweli wa kauli hili. **(alama 10)**

**SEHEMU B: TAMTHILIA: BEMBEA YA MAISHA – TIMOTHY AREGE**

**Jibu swali la 2 au la 3.**

**2**.Basi tu!Wenzenu ndio **waliioniingiza kwenye mkondo huu.**Kama unakumbuka nilikuwa miongoni mwa vijana kwanza kuingia kwenye dini.Hata tulikuwa tunahubiri.

(a).Fafanua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b).Tambua kwa kutolea mfano wa toni inayojitokeza katika muktadhaa huu**.(alama 2).**

(c).Tambua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili**.** **(alama 2).**

(d).Kwa kurejelea mifano mbalimbali eleza madhara au matokeo ya maneno yaliyopigiwa mstari katika tamthilia hii kwa jamii husika**.** **(alama12)**

**Au**

**3.** Fafanua mabadiliko yanayojitokeza katika tamthilia ya Bembea ya maisha (alama 20)

**SEHEMU YA C :HADITHI FUPI**

***MAPAMBAZUKO YA MACHWEONA HADITHI NYINGINE***

***Jibu swali La 4 au 5***

**WINNIE NYARURI OGENCHE:SABINA**

**4** .Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.

**a)**Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. **(alama 6)**

**b)**Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. **(alama 4)**

c)Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. **(alama 10)**

**5.** Kwa kurejelea hadithi zozote tano jadili changamoto zinazoikabili sekta ya elimu**. (alama 20)**

**SEHEMU YA D USHAIRI**

***Jibu swali la 6 au la 7***

***6 Soma shairi lifuatalo kasha ujibu masuali***

Naogopa, kukupa wangu mtima, sitaki mie nilie
Naogopa, kutoa yangu kalima, eti wewe utulie
Naogopa, ninashindwa kusimama, wewe pete unitie
Naogopa, wanaume wanauma, ja panya wapulizie.

Naogopa, kwita wako mama mama, nami anikaripie
Naogopa, sipendi nyingi dhuluma, za wanaume nilie
Naogopa, kushinda nimeinama, goti mume nipigie
Naogopa, za mkemwenza hujuma, matusi anipatie.

Naogopa, uchungu ukiniuma, mwana nikakuzalie
Naogopa, kupigwa kama ngoma, ndiposa nikatulie
Naogopa, kila kitu kunisoma, ndo hela unipatie
Naogopa, kuitwa mwizi wa sima, ila nikuandalie.

Naogopa, dadazo kuwaandama, udaku wakanitie
Naogopa, kuuleta uhasama, mimi mnipiganie
Naogopa, koritini kusimama, mali tukashindanie
Naogopa, kumwaga wenu mtama, kuku niwamiminie,

Naogopa, naogopa ninasema, yabidi uvumilie
Naogopa, nawe babu kusimama, eti ndoa niingie
Naogopa, ndoto zangu kuzizima, hili doa nijitie
Naogopa, taa yangu kuizima, mwingine jitafutie.

**MASWALI**

**a)** Lipe shairi hili anwani mwafaka. **(Alama 1)**
**b)** Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili**.** **(Alama 1)**
**c)** Nani nafsi nenewa katika shairi hili? **(Alama 1)**
**d)** Taja tamathali za lugha zilizotumika katika shairi hili. **(Alama 2)**
**e)** Fafanua uhuru wa ushairi alioutumia malenga. **(Alama 2)**
**f)** Weka shairi hili katika bahari mbalimbali**.** **(Alama 3)**
**g)** Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. **(Alama 4)**
**h)** Kwa nini nafsi neni anasita kuchukua hatua? **(alama 4)**
**i)** Vifungu vifuatavyo vina maana gani katika shairi**?** **(alama 2)**
 **i.**Taa yangu kuizima
 **ii.**Dhuluma

***Au***

***7  Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisha kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu,
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa,
Iwapo wewe ni mume,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!

Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri

**Maswali**

**(a)** Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha. **(alama 2)**
**(b)** Ni nani anayeimba shairi hili na analiimba kwa nani ? **(alama 2)**
**(c)** Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi ya kiume. **(alama 2)**
**(d)** Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili **(alama 4)**
(e) Taja shughuli zozote **mbili** za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili. **(alama 2)**
(f) Eleza kwa mifano, uhuru wa kishairi katika shairi hili **(alama 4**
(g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? **(alama 4)**

(i) Mbari
(ii) Msununu
(iii) Ngariba
(iv) Uvundo

**1) FASIHI SIMULIZI.**

**Soma kifungu kifwatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Mwanangu, masomo ni jambo muhimu sana. Utakapofika chuoni na kuanza maisha ya chuo kikuu, tafadhali usijiingize katika mambo ya dunia; anasa na raha nyingi. Vitabu view rafiki wa karibu. Jaribu kusaidiana na wenzako na utie bidii za mchwa masomoni.

Mwanangu kumbuka elimu ndio ufunguo wa maisha mema hapo usoni. Isitoshe safari yako ya maisha mema usoniunaanza uifikapo kule. Jiepushe na mambo mabaya ili usiangukiwe na mti.

**Maswali**

**a)** Kwa kutolea mifano, tambua kipera hiki. **(alama 2)**
**b)** Bainisha sifa za kipera hiki **(alama 5)**
**c)** Tambua nafsi neni na nenewa katika kipera hiki. **(alama 2 )**
**d)** Fafanua vipengele muhimu katika kufanikisha uwasilishaji wa fasihi simulizi. **( alama 5)**
e). Wewe ni kati ya wanaotambiwa hadithi katika mandhari maalum. Fafanua mambo ambayo wewe na wenzako mnaweza kuchangia wakati wa utambaji**.** **(alama 6)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 5

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

JINA………………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

1. *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
2. *Kisha chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.*
3. *Kila insha isipungue **maneno 400***
4. *Kila insha ina **alama 20***
5. *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**MASWALI**

**1.** Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la ***Taifa Leo.***

Andika barua ya kuomba nafasi hii na uiambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi.

**2.** *Jukumu la kuzuia msambao wa **virusi vya korona** ni la mtu binafsi.* Jadili.

**3.** Andika insha itakyothibitisha ukweli wa methali

Mchelea mwana kulia, hulia mwenyewe.

**4.** Anza kwa.

Mwanangu, dunia imebadilika pakubwa lakini chunga mabadiliko hayo yasikuzuzue**….**

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 5

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………………  SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**MUDA SAA 2 ½**

*Jibu maswali yote, majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

**1. UFAHAMU (Alama 15)**

Huku ulimwengu unapoingia ya katika teknologia ya tarakilishi na sera ya utandaridhi, ukweli wa mambo ni kuwa akina mama wamezinduka. Suala la usawa wa kijinsia limeanza kushamiri kote duniani na ole wake mwanamume yeyote ambaye hajawa tayari kutembea na majira. Lakini hebu tuchunguze jambo hili kwa makini zaidi.

Usawa wa jinsia ni nini? Usawa wa kijinsia ni usawa wa binadamu wote; wawe wake au waume. Usawa huu unapaswa kudhihirika katika kugawa nafasi za kazi, utoaji wa elimu, nafasi za uongozi na Nyanja zinginezo zozote za maisha.

Ubaguzi wa aina yoyote ile hasa dhidi ya mwanamke ni jambo linalokabiliwa na vita vikali sana ulimwenguni kote.

Dahari na dahari, hasa katika jamii za kiafrika kumekuwa na imani isiyotingizika kuwa mwanamke ni kiumbe duni akilinganishwa na mwanaume. Kwa hivyo mwanamke amekuwa akifanyiwa kila aina ya dhuluma ikiwepo kupigwa, kutukanwa, kudharauliwa, kunyimwa haki zake, kunyimwa heshima na mambo kama hayo, lakini je, ni kweli kuwa mwanamke ni kiumbe duni asiyefaa kutendewa haki?

Tukichunguza jamii kwa makini tunaweza kuona mara moja kuwa hivyo ni imani potovu isiyo na mashiko yoyote. Ukimulika familia yoyote ile iliyopiga hatua kimaendeleo, uwezekano mkubwa ni kuwa mume na mke wa familia inayohusika wana ushirikiano mkubwa. Mume anamthamini mke wake na <u>hadiriki</u> kufanya maamuzi muhimu yanayoweza kuathiri maendeleo ya familia bila kumhusisha mke. Mume kama huyo huketi na mkewe, wakishauriana na kufikia uamuzi bora.

Tukitoka katika muktadha wa kifamilia na kumulika ulimwengu wa kazi iwe ni katika afisi za serikali au kwenye makampuni binafsi, ukwerli ni kwamba kiongozi yeyote yule aliyefaulu katika usimamizi wake mara nyingi huwa na mke nyumbani ambaye wanashauiriana kila uchao kuhusu kazi anayofanya hata kama mke hafanyi kazi mahali pale. Hisia na mawaidha anayotoa mke kwa mume wake ni tunu na huenda asiyapate kwingineko kokote hata katika vitabu vya kupigiwa mifano. Hii ni mojawapo ya sababu ambayo huwafanya viongozi wa nchi mbalimbali kupenda sana kuwatambulisha wake na familia zao waziwazi kwa vile wanajua kuwa jamii inathamini sana msingi wa jamii. Kiongozi ambaye hana mke au familia au yule ambaye hana mke wake hatambuliki, hutiwa mashaka na jamii hata kama ni kiongozi aliye na azma ya kushikilia kazi ngumu ya kuongoza umma.Tukirudi nyuma kidogo na kupiga darubini mataifa ya mbali, tunaweza kuwaona wanawake mashuhuri walio uongozini ambao hadi waleo unapigiwa mfano. Wanawake mashuhuri waliotoa uongozini ambao hadi wa leo unapigiwa mfano. Wanawake hao walisimamia mojawapo ya mataifa yenye uwezo na ushawishi mkubwa Zaidi duniani. Ingawa wengi wao sasa wameng'atuka, uongozi wao bado unakumbukwa hata baada ya miaka mingi ya wao kuamua kupumzika ,mfano ni kama :Bi Bandranaike wa Sri lanka, Golda Meir wa Israel na wengine wengi katika mataifa kama Indonesia, Ufilipino, Bangladesh, Pakistani na kwingineko.Katika kufikia tamati, tunapozungumza kuhusu jinsia, hatuna budi kugusia kitafsili masuala nyeti. Kwanza,imani ya kushikilia kikiki tamaduni zisizofaa, ni jambo

linalofaa kuchunguzwa kwa makini. Kwa mfano, kuna badhi ya jamii ambazo humlazimu mke kurithiwa baada ya kifo cha mumewe. Vile vile baadhi ya jamiii za kiafrika zinanshikilia kuwa mwanamke hana haki ya kurithi. Kutokana na Imani hii, wanawake wengi huishi maisha ya taabu baada ya kutengana na waume zao kwa vile hawana haki ya kurithi chochote kutoka kwa wazazi wao hata kama wazazi hao wana mali nyingi kupindukia. Mali ya wazazi ni haki ya watoto wa kiume wala si watoto wa kike! Hili ni jambo la kusikitisha mno.

Isitoshe, wanawake hukumbukwa na kizingiti kingine wanapojaribu kumiliki mali ya waumezao baada ya waume hao kukata kamba .sababu ni kuwa,baada ya hao wenda zao kuwekwa kaburini, vita vya umiliki wa mali huanza mara moja na mwishowe yule mke maskini hujikuta hana hata mahali pa kulala sembuse mali waliyochuma na mali yake yote kunyakuliwa na aila ya mumewe . Jambo hili linaonyesha namna tulivyoachwa nyuma na uhalisia wa mambo. Ni lazima jamii izuinduke na itoke kwenye kiza hiki chenye maki nzito.

**MASWALI**

**a.** Ina maana gani kusema kuwa wanaume hawana budi “kutembea na majira” **(alama 2)**

**b.** Kabla ya uzinduzi huu kuhusu usawa wa jinsia, wanawake wamekuwa wakitendewa dhuluma za kila aina. Taja tatu. **(alama 3)**

**c.** Je, ni kwa nini viongozi wengi hupenda kujitambulisha na familia zao? **(alama 2)**

**d.** Je, unaamini kuwa hisi na mawaidha anayatoa mke wa mume wake ni tunu na huenda yasipatikane kwingineko? Fafanua **(alama 2)**

**e.** Je, licha ya kunyimwa haki yake ya kujiamulia, ni matatizi yapi mengine yanayoweza kumkumba mke anayelazimishwa kurithiwa? **(alama 3)**

**f.** Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika hali muktadha. **(alama 3)**

Kushamiri

Hulka

Azma

**2. MUHTASARI**

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo.*

Idadi kubwa ya wanafunzi huingiwa na wasiwasi wakaribiapo kufanya mtihani kwa sababu mbalimbali, kubwa likiwa ni hofu kwa jinsi ambavyo watafanya katika mtihani huo. Asilani mambo hayafai kuwa hivyo. Wataalamu wa masuala ya saikolojia na wale wa elimu wanashauri kuwa mtahiniwa anafaaa kupata muda mwingi wa mapumziko wakati anapokaribia kufanya mtihani ili aweze kuituliza akili asije akapatwa na mzongo wa akili.

Moja katika mashauri ni kuwa mtahiniwa anafaa kupata usingizi wa kutosha wakati akijiandaa na pia wakati akifanya mtihani. Hii ni kwa sababu mtihani wa mwisho si tofauti na mitihani mingine

ambayo mtahiniwa amekuwa akifanya, pamoja na kuwa ni maswali ya jumla tu kutoka viwango vyote vya masomo. Hivyo basi, mtihani unapokaribia, mtahiniwa anafaa kudurusu na kufanya majaribio mbalimbali ya mtihani pamoja na kujikumbusha yale aliyofunzwa na mwalimu wake. Wale asimdunishe au kumdharau mwalimu hata kama stadi zake za kufundisha kazikumsisimua – alikupa kito cha thamani kitakachokufaa kama silaha wakati wa mtihani.

Mtihani unapokaribia, mtahiniwa anafaa kuwa amekwisha kutambua udhaifu wake na kutia bidii kuudhibiti kupitia udurusu, mijadala na mashauriano. Kumbuka kuwa bidii haiui ila hulipa. Hivyo basi, kila unaposhirikisha bidii na ujasiri wa wako na kuimarisha uelewe wako wa somo, na hatimaye ukaboresha matokeo katika somo hilo. Vilevile, kujadili au kufafanua mada unayoielewa vyema kwa m wenzio aiyeielewa kutakuwezesha kuielewa hata Zaidi na hivyo kuimarisha uwezo wako wa kuzoa alama nyingi katika mtihani endapo swali litatoka katika mada hiyo.

Pamoja na hayo, mtahiniwa anafaa kujihadhari na majuto ya kufanya kile ambacho hakupaswa kufanya. Anaweza kuhakikisha hili kwa kuyapitia maswali kwa makini Zaidi, na kuyatafakaria, kuyapangia na kuaandikia majibu sawasawa kasha kuyasoma tena majibu yake ili kuwa na uhakika kwamba hajapotoka.

Ikiwezekana (kwa sababu ya tofauti za kimapato na uwezo wa wazazi au walezi) mtahhiniwa anafaa kula visuri kabla kuenda kufanya mtihani. Vilevile, anapaswa kufika katika chumba cha mtihani kwa wakati unaofaa – mapema kabla ya muda wa kuanza kwa mtihani – na ahakikishe amebeba kila kifaa atakachokihitaji katika mtihani huo.

Ikiwa utashindwa kujibu swali Fulani, usipotezee muda mwingi. Baadala yake, enelea na swali linalofuatia kasha ulirejelee swali lile lililokutatiza baadaye ukishamaliza maswali yale mengine. Usipoteze muda kutafuta jibu ambalo huna kwa wakati huo. Juu ya yote, usidhubutu kuifanya hila katika mtihani kwa kuwa kitendo kama hicho kitasababisha matokeo yako kufutiliwa mbali, nayo bidii yako ya miaka mine itakuwa imeishia gizani, ukasalia kujuta.

**Maswali.**

**a)** Tumia maneno 60 kueleza ujumbe ulio katika aya mbili za mwanzo. **(alama 6)**

**Nakala chafu**

**Jibu**

**b)** Mwandishi anatoa ushauri gani kwa mtahiniwa katika aya ya tatu hadi ya mwisho? Eleza kwa maneno 100 **(alama 9)**

**Nakala chafu**

**Jibu**

## SEHEMU C - MATUMIZI YA LUGHA.

**(a)** Eleza ufauti ya kimsingi iliyopo kati ya irabu na konsonanti. **(ala2)**

**(b)** Taja sifa tatu bainifu za irabu /O/ **(ala 3)**

**(c)** Andika maneno yenye muundo ufuatao **(ala2)**

**i)** KKKIKI

**ii)** KKIKI

**(d)** Andika tungo ya neno moja yenye viambishi vifuatavyo.

**i)** Nafsi

**ii)** Njeo

**iii)** Kirejeshi

**iv)** Shamirisho

**v)** Mzizi

**vi)** Kauli ya kufanyiza

**vii)** Kiishio **(ala3)**

**(e)** Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeana**.** **(ala2)**

i) –la

ii) – nywa

---

**(f)** Andika sentensi ifuayo kulingana na maagizo. **(ala2)**

**Maagizo**

Mhalifu alisamehewa kwa sababu alinyenyekea .

Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino.

**(g)** Andika kwa wingi

Kelele ya amchaye Mungu ni baraka. **(ala1)**

**(h)** Tambua aina ya vishazi katika sentensi hii

Utazawadiwa ukicheza vizuri. **(ala2)**

**(i)** Tofautisha matumizi yapo katika sentensi hizi. **(ala2)**

1. Alipomwona alimhoji.
2. Amwonapo humhoji

**(j)** Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari. **(ala2)**

Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa mno na viongozi wenye msimamo thabiti mno.

**(k)** Unda nomino kutokana na vitenzi **(ala2)**

1. Jaribu

2. Chuma

**(l)** Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi

Wageni na wenyeji walikimbiliana **(ala 2)**

**(m)** Andika katika msemo wa taarifa. (ala3)

"Nitakuarifu nikimwona" Maria alisema

**(n)** Eleza maana mbili za sentensi **(ala2)**

Tuliitwa na Juma

---

**(o)** Tumia "0" rejeshi katika sentensi ifuatayo

Mtu ambaye hutupa tope hujichafua mwenyewe. **(ala 2)**

**(p)** Tumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika tena sentensi ifuatayo.

Ukuta umemwuumiza mvulana alipokuwa akiuparaga. **(ala3)**

**(q)** Changanua sentensi kwa njia ya jedwali.

Ouma alianguka mtihani ila Kamau alifuzu vizuri. **(ala4)**

## ISIMU JAMII

Mtu 1: Wewe njoo hapa (kwa sauti kubwa) fanya upesi.
Mtu II : (anakimbia mbio) Naja Sir
Mtu I : (anamtazama) unajifanya mwelevu?
Mu II : Hapana Sir……eh…..afande
Mtu I : Jina
Mtu II : Samwel Kioko
Mtu I : (Huku akiandika) Lete kitambulisho
Mtu II : Sina hapa sir
Mtu I : Huna kitambulisho? Utafanyiwa booking vipi?
Mtu II : Naomba
Mtu I : Naomba ! naomba! Unaomba nini? Wazururaji kama nyinyi tunawajua. Mnajifanya hamjui kuna curfew. Mnajiponza, "zerikali saidia". Usiniharibie muda wangu (akiashiria) ingia ndani! Utakuwa mgeni wetu leo. Tutakukarimu chakula cha chumba.(anamsukuma ndani)

**a)** Bainisha sajili ya makala haya. **(ala2)**

**b)** Eleza sifa nne za sajili kwa kurejelea makala haya. **(ala 8)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 5

**102/3**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 3

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE……………………………………………… SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

***a)*** *Andika jina lako, shule, nambari ya mtihani kisha utie sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
***b)*** *Jibu maswali manne pekee*
***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima*
***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | JUMLA | |

**SEHEMU A: USHAIRI**

**1**.Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata. **(alama 20)**

**TENDA BILA UZIMBEZIMBE!**

Natakadamu kulonga , longa nawe pia longa,
Longalonga ukipinga , pinga ukunguni pinga,
Pingapinga ukipanga , panga ya kutenda panga,
Amali tenda bila uzimbezimbe.

Kazi ukipata tenda, tenda ndugu yangu tenda ,
Tendatenda kwa kupenda , penda kwa khatari penda,
Pendapenda na kupanda , panda nia njema panda,
Amali tenda bila uzimbezimbe.

Vinyago ‘ kiweza chonga, chonga kwa makini chonga,
Chongachonga ukifunga, funga midomoyo funga,
Fungafunga ukichunga , chunga gange yako chunga ,
Amali tenda bila uzimbezimbe.

Wimbo nimtamu imba , imba kwa naghama imba,
Imbaimba ukipamba, pamba kiufundi pamba
Pambapamba ukiamba, amba ya heshima amba,
Amali tenda bila uzimbezimbe.

Uwapo muwashi jenga , jenga nyumba nyingi jenga,
Jengajenga ukienga, enga muwanzoni enga ,
Engaenga ukilenga , lenga ufanisi lenga,
Amali tenda bila uzimbezimbe
Kuni upatapo chanja, chanja kwa furaha chanja,
Chanjachanja ukionja, onja pato lako onja ,
Onjaonja ukivunja, vunja wazo jiwi vunja,
Amali tenda bila uzimbezimbe

Tungo nakoma kutunga, tunga ukiweza tunga ,
Tungatunga ukilinga , linga vina vyake linga,
Lingalinga ukiwanga, wanga mizanize wanga,
Amali tenda bila uzimbezimbe.
(Malenga wa Ghuba, Fred Obondo)

**Maswali**

a)Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili. **(alama 2)**
b)Eleza umbo la shairi hili **(alama 4)**
c) Kwa kutolea mifano, eleza aina mbili za uhuru wa kishairi katika shairi hili **(alama 2)**
d) Taja kwa kutolea mifano mbinu mbili za lugha katika shairi hili . **(alama 2)**
e)Eleza ujumbe wa shairi hili **(alama 4)**
f) Eleza toni ya shairi **(alama 2)**
g) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari **(alama 4)**
h) Eleza maana ya kibwagizo cha shairi hili **(alama 2)**

**SEHEMU B – RIWAYA – NGUU ZA JADI – CLARA MOMANYI**

**2**. ‘’Anataka kubakia uongozini ili azidi kuwanyanyasa na kuwapoka haki zenu.’’
i) Eleza mkutadha wa dondoo hili **(alama 4)**
ii) Eleza sifa mbili za mhusika msemaji **(alama 2)**
iii) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kujenga ploti ya hadithi hii **(alama 2)**
iv) Kwa kurejelea hadithi hii , jadili mbinu alizotumia mrejelewa kuendelea kubaki mamlakani **(alama 10)**

au

**3**.Kwa kutoa idhibati, jadili ufaafu wa anwani Nguu za jadi **(alama.20)**

**SEHEMU YA C – TAMTHILIA - BEMBEA YA MAISHA - TIMOTHY AREGE**

**4.**’’Kumbe watoto hawa tuliowadharau walikuwa nyota ya jaha.Sasa kijiji kizima kina mwanga .’’
**i)**Thibitisha namna watoto hawa wamekuwa mwanga kwa kijiji hiki **(alama 10)**
**ii**) Eleza umuhimu wa msemaji **(alama 4)**
**iii**) Jadili namna mwandishi ametumia mbinu ya taswira kujenga maudhui katika tamthilia ya bembea ya maisha. **(alama 6)**

**D . HADITHI FUPI – MAPAMBAZUKO YA MACHWEO**

**5.a)**Sasa mbona wamkaribisha humu mwako nyumbani kila anapobisha ? anapokukebehi na kututafishi hapa mbona unamvumilia ? Hana shukrani yule ! Mwepuke na ujishughulishe na yako,……….. mbona hunielewi ? …………..
**i)**Eleza mkutadha wa dondoo hili . **(al.4)**
**ii**)Changanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili . **(al.4)**
**b)i**) Eleza toni inayojitokeza katika dondoo hili **(al.2)**
**iii**)Dondoo hili linaonyesha migogoro katika jamii . Toa mifano mitatu ya migogoro inayojitokeza **.** **(al.6)**
**iv**)Onyesha namna msemaji anachangia kujenga ploti katika hadithi hii. **(al.4)**

au

**c)**Kwa kurejelea hidithi zifuatazo , jadili jinsi waandishi wamemsawiri/ wamemchora mwanamke **.** **(al.20)**
**i)** Sabina

**ii**) Nipe nafasi .

**E. FASIHI SIMULIZI**

**6.a)** Usiwe na pupa mwanangu , Pupa haifikishi mtu popote. Badala yake huharibu , sikiliza mwanangu . Wazazi wako walipoana, walikaa sana bila kupata mtoto . Hakuna daktari ambaye hakujaribu kutegua kitendawili cha wao kupata mtoto. Mwishowe babako akataka kumpa mamako talaka . Wazee nyumbani walimhimiza aoe tena . Lakini mimi nilimshauri asimtupe mkewe . Alinisikia maana tumekuwa marafiki wa jadi . Mamako akapatwa na mughma mkubwa . Hakujua aokote wapi mtoto.

**i**) Tambua kipera cha maelezo haya **(al.2)**

**ii)**Eleza sifa mbili za kipera hiki **(al.4)**

**iii)** Jadili majukumu manne ya kipera hiki **(al.4)**

**b)i**) Taja na ueleze sifa mbili kuu za mtambaji bora wa fasihi simulizi **(al.4)**

**ii)** Onyesha baadhi ya matatizo yanayokumba utafiti na uhifadhi wa fasihi simulizi **(al.6**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 6

**102/1**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 1

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA…………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………………  SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI……………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima*** *kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

***b)*** *Kila insha isipungue maneno 400.*

***c)*** *Kila insha ina alama 20.*

***d)*** *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

***Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee***

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| **Jumla** | **40** | |

# INSHA

**SWALI LA LAZIMA**

**1.** Kama mhariri wa gazeti, andika **tahariri** ukipongeza hatua ya serikali kupiga marufuku matumizi ya karatasi za sandarusi.

**CHAGUA MOJA:**

**2.** Eleza njia za kustawisha uchumi uliosambaratika katika eneogatuzi lako.

**3.** Pwagu hupata pwaguzi.

**4.** **Andika** insha itakayomalizikia kwa maneno haya.

**"…**Nilipokaa mezani kula chakula kitamu, nilikumbuka maisha magumu niliyoyapitia, nikatambua kuwa si rahisi kupata chakula kama hicho bila juhudi maishani**"**

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 6

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

JINA………………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- *Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Weka **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa*
- *Jibu maswali yote.*
- *Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |

**1. UFAHAMU:** **(ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**:

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi – vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitisha hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahabu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano,

hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kinga zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na, ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

**Maswali**

**a)** Yape makala haya kichwa. **(alama 2)**

**b)** Mbali na athari kwa uzazi kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. **(alama3)**

**c)** Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. **(ala 4)**

**(d)** Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu. **(alama 2)**

**(e)** Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. **(alama 3)**

**(f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa. **(alama 1)**

Gandwa

**2. UFUPISHO:** **(ALAMA 15)**

**<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali</u>**:

Biashara ya kimataifa ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile. Nchi mbalimbali zimekuwa zikitegemeana kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, nchi ya Kenya imekuwa ikiuza maua na mboga katika nchi za ng'ambo na kupata fedha za kigeni ambazo hutumiwa humu nchini kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Biashara ya kimataifa huziwezesha nchi ambazo hazizalishi bidhaa na hata huduma mbalimbali kupata bidhaa hizo kutoka nchi nyingine zinazohusiana nayo katika biashara. Mathalan, Kenya ni nchi ambayo imekuwa ikitegemea kilimo lakini haijaendelea katika sekta ya viwanda. Kenya huagiza bidhaa kama vile vipuri vya magari na hata magari yenyewe kutoka nchi kama vile Japan. Nayo Kenya huuza mazao ya shambani kama vile pareto, chai na kahawa ng'ambo.

Kupitia kwa biashara ya kimataifa, nchi hupata masoko kwa bidhaa zake. Kwa vile biashara ya kimataifa huziwezesha nchi husika kuzalisha bidhaa mahususi ambazo hazitaigharimu nchi pesa nyingi kuzalisha, nchi hizo aghalabu huzalisha kiasi kikubwa cha bidhaa kuliko mahitaji yake ya nyumbani. Nchi basi hulazimika kutafuta masoko nje ya mipaka yake. Kwa njia hii uchumi wa nchi huendelea kuimarika.

Aidha, biashara ya kimataifa huwezesha nchi kupata huduma za kitaaluma ambazo hazipatikini katika nchi husika. Kuna nyanja za kiuchumi ambazo huhitaji wataalamu mahususi. Kwa mfano,

katika sekta ya matibabu nchini humu tumepata kwamba kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanahitaji matibabu maalumu. Wanaougua magonjwa haya huagiziwa madaktari kutoka ng'ambo au hata kupelekwa ng'ambo kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

Biashara ya kimataifa hukuza ushirikiano wa kimataifa. Nyakati za majanga ya kimaumbile na hata mengine yanayosababishwa na kutowajibika kwa binadamu, nchi hupata usaidizi kutoka nchi za ng'ambo. Kwa mfano wakati wa mkasa wa bomu wa 1998, Kenya ilipata msaada wa kukabiliana na janga hili kutoka Israeli, Marekani na hata Ujerumani ambako baadhi ya waathiriwa wa mkasa huo walipelekwa kwa matibabu zaidi. Ushirikiano huu wa kimataifa huwezesha wananchi kutoka nchi fulani kwenda kusomea na hata kufanya kazi katika nchi nyingine. Katika miaka ya hivi karibuni Wakenya wengi wamekuwa wakienda kusomea vyuo vikuu vya ng'ambo. Wengine wamediriki kupata kazi katika mashirika ya kimataifa katika nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Rwanda, Msumbiji na kadhalika.

Biashara ya kimataifa husaidia kukuza ushindani kati ya nchi husika. Ushindani huu ni hakikisho la uzalishaji wa bidhaa za thamani bora. Kila nchi itafanya juu chini kuzalisha bidhaa ambazo zinaweza kukubalika katika soko la kimataifa. Pia wananchi wa nchi husika hupata aina tofauti za bidhaa badala ya kutegemea aina moja tu ya bidhaa zinazozalishwa nchini mwao.

Biashara ya kimataifa huleta ushirikiano wa kisiasa na uelewano zaidi kati ya madola mbalimbali. Mathalan muungano wa nchi za Afrika Mashariki – Kenya, Uganda na Tanzania, hauchangii tu kuleta manufaa ya kiuchumi bali huleta ushirikiano zaidi wa kisiasa.

Ingawa biashara ya kimataifa ina natija, biashara hii huandamana na hasara mbalimbali. Biashara hii imesababisha kuwapo kwa masoko huru ambayo yameleta ushindani mkubwa kwa wafanyibiashara wadogo wa humu nchini. Baadhi ya wafanyibiashara wamelazimika kufunga biashara zao baada ya kufilisika. Ushuru mkubwa unaotozwa baadhi ya bidhaa nchini huwafanya wananchi wengi kutofaidika kwa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, kuna ucheleweshaji wa bidhaa zilizoagizwa. Bidhaa hizi mara nyingi huchukua muda kabla ya kutoka nchini, kwa hivyo wafanyibiashara wengi hulazimika kungojea kupata bidhaa hizi na kuwauzia wateja wao.

Vilevile, kutokana na biashara ya kimataifa, bidhaa duni huweza kupenyezwa katika mataifa yanayoendelea. Pia baadhi ya wafanyibiashara wa kimataifa huchukua fursa hii kulangua dawa mbalimbali za kulevya ambazo huwaathiri vijana wa nchi husika. Wengine huhusika katika vitendo vya kigaidi kama vile uchomaji wa majengo mbalimbali kwa bomu na mauaji ya ananchi wasio na hatia.

Ni kweli kuwa biashara ya kimataifa ina hasara zake. Hata hivyo mhimili mkubwa wa uchumi wa mataifa machanga.

**(a)** Kwa maneno yasiyozidi **themanini**, eleza umuhimu wa biashara ya kimataifa. **(alama 7)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**(b)** Kwa maneno yasiyozidi **40**, eleza ujumbe wa aya tatu za mwisho. **(alama 6)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** Sahihisha sentensi: **(alama 2)**

(i) Mitume hiyo siyo ambayo tunaijua.
(ii) Wasikilizaji sasa wanaburudika na muziki kutoka idhaa la taifa hii.

**(b)** Ikanushe sentensi hii katika umoja. **(alama 2)**
Wasingecheza kiustadi wasingeshinda katika michezo ile.

**(c)** Tambulisha nyakati na hali katika sentensi: **(alama 2)**
**(i)** Wachezaji walikuwa wanafanya mazoezi.
**(ii)** Nkirote alipoingia alitukemea.

**(d)** Eleza maana za sentensi. **(alama 2)**
**(i)** Kwa nini wasililie hapa?
**(ii)** Kwa nini wasilie hapa?

**(e)** Toa mifano miwili miwili ya sauti zinazotamkiwa katika : **(alama 2)**
**(i)** ufizi ……………………………………………………………………
**(ii)** meno ……………………………………………………………………

**(f)** Andika udogo na ukubwa wa neno 'kidole'. **(alama 2)**

**(g)** Tunga sentensi mbili tofauti kubainisha matumizi ya KWA. **(alama 2)**

**(h)** Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**
Msichana alimkaririra mgeni shairi.

**(i)** Tumia vitenzi hivi katika sentensi mojamoja katika jinsi ya kufanyiwa. **(alama 2)**
**(i)** nywa
**(ii)** pa

**(j)** Kistari kifupi ( - ) aghalabu hutumika kuendeleza sauti hasa katika vihisishi. Onyesha matumizi mengine matatu ya alama hii akifishi. **(alama 3)**

**(k)** Tunga sentensi kubainisha tofauti kimaana kati ya vitawe: **(alama 2)**
**(i)** juha……………………………………………………………………………………
**(ii)** jua……………………………………………………………………………………

**(l)** Ziandike upya sentensi hizi kwa mujibu wa maagizo uliyopewa. **(alama 2)**
(i) Kiyondi aliukomelea mlango alipovisikia vishindo.
(Anza kwa :Mlango…………………..)
(ii) Mvua ilinyesha sana alasiri hiyo. Wachezaji walicheza mpira vizuri tu.
(Tumia 'japo')

**(m)** Tunga sentensi sahihi kubainisha matumizi ya <u>KI</u> kuonyesha: **(alama 4)**
**(i)** masharti
**(ii)** ngeli
**(iii)** kufanyika vitenzi viwili au zaidi wakati mmoja
**(iv)** kielezi namna

**(n)** Tambua hali na matumizi ya kisarufi ya neno lililopigwa mstari katika sentensi: **(alama 1)**
Mtu <u>mzee</u> anapaswa kuheshimiwa

**(o)** Andika katika usemi halisi. **(alama 2)**
Mwalimu aliwaagiza wanafunzi warudi darasani, warejelee madaftari yao ya kumbukumbu na kuikosoa kazi hiyo.

**(P)** Andika katika umoja. **(alama 2)**

Tembe ambazo tulizimeza zilikuwa chungu.

**(q)** Eleza maana za semi au nahau: **(alama 2)**

**(i)** kwenda mbweu

**(ii)** shika sikio

**(r)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali **(alama 4)**

Kiatu kilichonunuliwa juzi kimerejeshwa dukani.

## 4. ISIMU - JAMII

**(a)** Eleza ukionyesha bayana tofauti baina ya lahaja na lafudhi. **(alama 4)**

**(b)** Taja sifa tatu tambulizi za lugha ya misimu **(alama 3)**

**(c)** Orodhesha sifa kuu za sajili ya siasa. **(alama 3)**

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 6

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE………………………………………………   SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- *Jibu maswali manne pekee. Swali la kwanza ni la lazima*
- *Maswali hayo mengine yachaguliw e kutoka sehemu zilizobaki*
- *Usijibu maswali **MAWILI** kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

## SEHEMU YA A: RIWAYA

***Clara Momanyi: NGUU ZA JADI***

**LAZIMA**

1. "Lakini mbona umeamua kunyamaza hivyo? Huoni watu wanakutegemea?" "…Wajua, kinywa kilichofumbwa hakiingii nzi."

a) i) Eleza **muktadha** wa dondoo hili. **(alama 5)**

ii) Tambua **toni** katika dondoo hili. **(alama 2)**

iii)Taja **mbinu moja** ya lugha katika dondoo kisha utoe mfano wa mbinu hii katika dondoo. **(alama 2)**

b)Mataifa mengi ya bara Afrika yanakumbwa na **matumizi mabaya ya mamlaka** ambayo ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya kiuchumi.Kwa kutolea mifano **kumi na moja** riwayani ya 'Nguu za Jadi',tetea ukweli wa kauli hii. **(alama 11)**

## SEHEMU YA B: TAMTHILIA

**Timothy Arege: Bembea ya Maisha**

*Jibu swali la 2 au 3*

2. Hata bembea ikiwa ya chuma hatimaye hulika.Wanasema papo kwa papo kamba hukata jiwe .Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo .Huungwa na mchezo kuanza tena.

a) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. **(alama 4)**

b) Jadili **umuhimu** wa msemewa wa maneno haya. **(alama 6)**

c) Kwa kutoa mifano mwafaka, tambua **mbinu tatu** za lugha ambazo zimejitokeza katika dondoo hili. **(alama 3)**

d) Baadhi ya wahusika katika tamthlia ya 'Bembea ya Maisha',bembea yao ilipokatika **haikuunganishwa tena hivyo basi mchezo haukuendelea, ulifika kikomo**. Onyesha ukweli wa kauli iliyokolezwa wino kwa kutolea mifano **saba** tamthliani. **(alama 7)**

***au***

3."Wanasema mlango mmoja ukifunga ,macho huiona mingine mingi iliyokuwa wazi ambayo awali yalikuwa hayaoni."

a) i) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. **(alama 4)**

ii) Eleza kwa kutolea hoja **nne** umuhimu wa mandhari katika tamthilia hii. **(alama 4)**

iii) Mnenewa ni mfano mzuri wa wahusika wasiokata tamaa maishani.Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja **sita** kutoka tamthiliani. **(alama 6)**

b) Jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa kwa mujibu wa tamthlia ya Bembea ya Maisha. **(alama 6)**

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

D.M.Lutomia na P.Muthama:***Mapambazuko ya machweo na Hadithi nyingine***

Douglas Ogutu*:***Toba ya Kalia**

**4. "**Asante sana kwa kitambulisho hicho.Natumai rafiki zako humu nchini wanafurahia popote walipo.Kwa niaba ya kituo hiki ninatoa shukrani kwako kwa kuitikia mwito wa kuwa nasi leo."

a) Eleza **nafasi ya vijana** kwa mujibu wa hadithi ya '**Toba ya Kalia**'. **(alama 6)**

b) "Hatutakukubalia kumdhalilisha mumeo,Moshe ndugu yetu kwa kuwatawanya watoto wake kwa kisingizio cha kutafuta kazi pasi na kibali kutoka kwa yeyote."

Kwa kurejelea hadithi ya '**Nipe nafasi**' jadili changamoto **sita** anazopitia mnenewa pamoja na wahusika wa jinsia yake. **(alama 6)**

Dominic Maina Oigo.**Kifo cha Suluhu**

c) Abigael alimaliza kusoma waraka ule huku machozi yakimbubujika kama maji kwenye maporomoko…Barua ile ilimfichulia siri si haba.

Thibitisha **kauli** iliyopigiwa mstari ukirejelea hadithi ya **Kifo cha Suluhu**. **(alama 8)**

***au***

**5.** D.W.Lutomia:**Msiba wa Kujitakia**

Jioni.Machoka ameketi kitako kochoni. Amerejea akiwa amechoka zaidi ya kuchoka. Pilkapilka zake za kutafuta kibarua mchana kutwa zimegonga mwamba.Hajui la kufanya. Matumbo yake yanateta kwa kushindwa kuhimili makali ya njaa. Hajatia chochote kinywani tangu asubuhi.Taswira ya chumba chake ingeweza kumliza kipofu! Anaweza juu ya maisha yake. Maisha ya wasakatonge.Maisha ya wanaojiita 'Pangu Pakavu'.Maisha ya wapiga kura. Maisha ambayo ni tofauti sana na maisha ya waliopigiwa kura.

Maisha kati ya makundi haya mawili yaani mpiga kura na mpigiwa kura, yametengana kama mbingu na ardhi.

Machoka anabaki kukondoa macho huku maonevu yakiihukumu nafsi yake.Anasimama pale kama kigingi.Hasongi wala kufurukuta.

a)Kwa kutolea mifano,fafanua **mbinu sita** za kimtindo katika fungu hili. **(alama 6)**

b) Dokeza **suala** ambalo linajitokeza katika maneno yaliyopigwa mstari. **(alama2)**

c) Onyesha namna Wanamatopeni wanavyokumbwa na **madhila** kwa kurejelea hadithi ya '*Msiba wa Kujitakia.*' **(alama 8)**

d) Fafanua **mbinu** nne za kutambua hulka/sifa za mhusika. **(alama 4)**

## SEHEMU YA D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au 7*

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Ni sumu, sumu hatari
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako leweshi
Za kupanda ngazi
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maneno laini
Ya ulimi wa mzazi

2.Ni sumu, sumu hasiri

3. Ni sumu, sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi
Ya daima kunywa 'moja band'
Mazoea mabaya ambayo
Ulevi
Yakufunga katika klabu
Hadi saa nane usiku baridi
Huku yakilenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi

4. Ni sumu, sumu jeruhi

Unajeruhi watoto kwa pesa
Kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika
Pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemichemi
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi

Unahasiri watoto
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
Zinawafikisha kwenye sigara na
Na kisha kwenya madawa
Ya kulevya
Barabara inayofikisha kwenye
Giza

La kaburi la asubuhi.

**Maswali**

a) Shairi hili ni la **aina** gani? Eleza. **(alama 2)**

b) Masuala kadhaa yamejadiliwa katika shairi hili.Fafanua yoyote **manne**. **(alama 4)**

c) Kwa kutoa mifano mwafaka ,tambua mbinu **mbili** za uandishi zinazojitokeza katika shairi hili. **(alama 4)**

d) Eleza **sura** ya shairi hili. **(alama 4)**

e) Andika ubeti wa **nne** kwa lugha tutumbi. **(alama 4)**

f) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi. **(alama 2)**

i) Jenga ukuta.

ii) Kwa pupa yako hangaishi.

***au***

**7**. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata*.

Ya wapi silika hino, ya kwenda kinyumenyume?
Nilijibu hata kwa wino, majibuyo niyasome,
Kuno 'geuza maneno, na kuyafanya maleme,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Insiya jilaani, ni bora wazi niseme,
Kukubalia idhini, mimba wakazikateme,
Hiyo nayo haki gani, wasiyoona mit ume,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Twajilaani laana, kijitakia ujume,
Nayo habari hatuna, twajiletea ukame,
Pia habari hatuna, ni wana sio vimeme,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.
Muswada siyo halali, wakuviavya vikembe,
Utawapea halali, mabinti wetu watambe,
Magulamu ja fahali, nao wakame pembe,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.
Kuavya mimba ni dhambi, ya kumuudhi Rahimu,
Laana twajaza tumbi, ya moto wa jahanamu,

Tuache vino vitimbi,turudie utimamu,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Jambo hili nawambia, litazidisha ukware,
Ni ya uvundo tabia, ni afueni tuisare,
Tuweze kuitubia, tuwache zino parare,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Muida ndio sinao, nina mengi ya kusema,
Wapigania hakio, zingatia nayosema,
'sipashe mswada huo , ni madhambi ya kuchoma,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

**Maswali**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. **(alama 1)**

b) Changanua shairi hili **kiarudhi**. **(alama 4)**

c) Kwa kutolea maelezo mwafaka,tambua **bahari tatu** za shairi hili. **(alama 3)**

d) Bainisha mbinu zifuatazo za kimtindo katika shairi hili: **(alama 3)**

i) Tashbihi

ii)Tanakuzi

iii) Swali balagha

e) Dhihirisha mtunzi huyu alivyofanikiwa kutumia **uhuru** wake kwa kutoa mifano **miwili**, kisha ueleze **umuhimu** wa kila uhuru ulioutambua. **(alama 4)**

f) Bainisha **toni** la shairi hili. **(alama 1)**

g) Fafanua masuala **mawili** ambayo yanazungumziwa katika shairi hili. **(alama 2)**

h) Bainisha aina **mbili za urudiaji** katika shairi hili. **(alama 2)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***Jibu swali la nane***

**8.a)** Nyimbo zina majukumu chungu nzima katika jamii.Kwa kutoa mifano mwafaka ya nyimbo hizi,fafanua majukumu **matano** ya nyimbo. **(alama 10)**

b) "Kama nguo yangu moja inachukua saa nne juani kukauka, je,nguo ishirini zitachukua muda gani?"

"Jibu - ni saa moja tu kwani zinatumia jua lile lile moja kukauka."

i) Tambua kijipera hiki. . **(alama 1)**

ii)Taja sifa za kijipera hiki. **(alama 4)**

c) Umekusudia kutumia mbinu ya **kushiriki** kufanya utafiti kuhusu tungo za aina hii. Eleza **manufaa matano** ya mbinu hii. **(alama 5)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 7

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

JINA……………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

*(a) Andika insha **mbili**.*
*(b) Insha ya kwanza ni ya **lazima** kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia*
*(c) Kila insha isipungue maneno **400***
*(d) Kila insha ni alama 20*
*(e) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**MASWALI.**

**1.** Wewe ni mwandishi wa habari. Umemwalika mwenyekiti wa tume ya utangamano na uwiano wa kitaifa nchini studioni ili kuangazia kwa kina swala la ukabila ambalo limekita mizizi katika taifa. Andika dayolojia kati yenu.

**2.** Nchi imekubwa na mizozo mingi ya kijamii hivi karibini. Huku ukipendekeza suluhisho, jadili vyanzo vya mizozo hiyo.

**3.** Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Nyumba njema sio mlango, ingia ndani uone.

**4.** Tunga kisa kitakachoanza kwa maneno yafuatayo: Giza lilikuwa limechukua milki ya viumbe wote duniani. Nyota zilitoa mwanga hafifu na mwezi ulikuwa ushatua. Katika giza hilo la kaniki**…**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 7

**102/2**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 2

**MUDA: SAA 2½**

JINA……………………………………………………………………………………

SHULE…………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
**b)** *Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
**c)** *Jibu maswali yote.*
**d)** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
**e)** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE:**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

**1. UFAHAMU**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Ikolojia ni elimu ya kisayansi inayohusu uhusiano wa kimazingira kati ya vitu vyenye uhai (mimea na wanyama) na visivyokuwa na uhai (hali ya hewa na udongo.)Sayansi ya ikolojia ipo katika mfumo wa elimu ya mazingira. Mfumo huu umegawanyika katika sehemu mbili: mfumo wa mazingira ya nchi na mfumo wa mazingira ya majini (bahari, maziwa, mito na madimbwi)

Viumbe wamejirekebisha kulingana na mazingira yao. Kwa mfano, samaki wana matamvua yenye uwezo na kusharabu hewa ndani ya maji. Ng’ombe wana mapafu ya kuvuta hewa katika nchi kavu. Sehemu za mvua ya kawaida zina mimea yenye majani makubwa ili iweze kuhifadhi maji nyakati za shida. Mimea ,wanyama,udongo na viathiri vingine vya hali ya hewa vinahusiana sana kimazingira. Mimea huota kutegemea hali ya nchi, umbo au sura ya ardhi na aina ya udongo.

Hali ya nchi ni wastani wa hali ya jotoridi, wastani wa mvua, unyevunyevu hewani, upepo, msukumo na mwanga kwa muda wa miaka thelathini. Dunia imegawanyika katika kanda mbalimbali. Kila kanda ina mimea na wanyama wa aina yake kutegemea hali ya nchi. Ukanda wa istiwai una joto, mvua na unyevunyevu mwingi. Miti ya ukanda huu hufanya misitu minene, yenye miti mirefu. Miti hii ni mirefu kwa sababu ya msongamano unaofanya miti igombanie mwanga wa jua kwa kurefuka. Katika misitu hii, ipo mimea ya kangaga inayotambaa na kukwea miti mingine. Katika ukanda wa Savanna hali ya joto na mvua si kubwa kama katika ukanda wa istiwai. Kwa sababu hii, sehemu nyingi ni vichaka na nyika zenye uwezo wa kuota nyasi zisizohitaji mvua.

Upepo una faida na hasara katika mazingira. Upepo husaidia kusukuma mawingu yaletayo mvua. Upepo unapozidi hudhuru mimea na wanyama kwa sababu hukausha maji ardhini, huvunja na kuharibu mimea, huleta vifo kwa wanyama na pengine kuharibu mazingira ya watu. Mimea katika mazingira hutegemea sana nuru ya jua ili kutengeneza chakula chake. Kiasi cha mwanga upatikanao mahali fulani huathiri mimea na wanyama wapatikanao katika mazingira yale.

## MASWALI

**(a)** Eleza dhamira ya mwandishi katika taarifa uliyoisoma **(alama 2)**

**(b)** Eleza maana ya Ikolojia **(alama 2)**

**(c)** Kwa nini wanyama huwa na sifa mbalimbali za kimaumbile? **(alama 2)**

**(d)** Ni kawa vipi Ukanda wa istiwai unatofautiana na ukanda wa Savanna? **(alama 2)**

**(e)** Ni kwa namna gani upepo unaweza kuwa na athari mbaya kwa mazingira? **(alama 4)**

**(f)** Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. **(alama 3)**

i. Matamvua_______________________________________________________________

ii. Kusharabu hewa_______________________________________________________

iii. Istiwai_____________________________________________________________

## 2. UFUPISHO

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya siasa baada ya uhuru, bali ni matokeo ya hali iliyokuwepo tangu enzi za mababu zetu; kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kisiasa kunaoana na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa siku nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi ilimwandaa mwanamke kuwa chombo kitiifu cha mwanamume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima wa malezi kuwa chombo cha kutumikia mwanamume-kumstarehesha, kumfariji, kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angeweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi naihusudu sana; ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya kijiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na ya wanaume pekee yao. Hakukuwa na mwanamke aliyeshirikishwa, hata kama alikuwa ajuza. Sifa waliyokuwa nayo wanawake ni ile ya usihiri na uganga. Mwanamke yeyote aliyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa wa uchawi, ulozi na ushirikina. Kwa hivyo, wanawake ndio waliokuwa washirikina wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara, alipuuzwa na pengine kutukanwa hadharani.

Kwa bahati nzuri, kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya. Vita vya wanawake vya kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia. Wanawake wengi wamekiuka misingi na mizizi ya utamanduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kumyanyasa na kumuumbua utu mwanamke tangu jadi. Watetezi wa haki za wanawake zamani walilaumu suala la serikali za mataifa mwaka hadi mwaka. Huku masuala ya wanawake ya kijamii, utu na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa, watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nchi moja. Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengine yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa, majukumu yao katika jamii, mfumo wa Umoja wa Mataifa wa wanawake na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya Umoja wa Mataifa miongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu.

Wanawake wameonyesha vipaji vyao katika nyanja mbalimbali za maisha; siasa, uchumi, utawala na kadhalika. Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na ya watu wengi. Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kuukubali ukweli huu, wapende wasipende. Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja na ya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi, wapinga mila na watovu wa utii.

**<u>MASWALI</u>**

**a)** Bila kubadilisha maana asilia, fupisha aya tatu za kwanza. (Maneno 45-55) **(Alama 6)**

**Matayarisho**

**Jibu.**

b) Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, pambanua hoja muhimu zinazoguziwa na mwandishi. (Maneno 60-65) **(Alama 9)**

**Matayarisho**

**Jibu**

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

**(a)** Andika neno lenye sauti zifuatazo**:** **(alama 1)**

Kipasuo hafifu cha midomo, irabu ya mbele wastani, kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya kati chini. ______________________________

**(b)** Tunga sentensi moja moja yenye aina zifuatazo za vishazi: **(alama 2)**

**(i)** Cha nia

**(ii)** Kitegemezi cha wakati

**(c)** Andika maana ya maneno yaliyopigiwa mstari. **(alama 2)**

Wali<u>sita</u> kufanya kazi hiyo baada ya saa <u>sita</u> usiku.

**(d)** Tia shadda: **(alama 2)**

i. pekee

ii. alinyongwa

(e)Huku ukitoa mfano, onyesha miundo mitatu ya maneno katika ngeli ya U-I **(alama 3)**

**f)** Tunga sentensi yenye vijisehemu vifuatavyo vya sarufi: **(alama 2)**

Kiambishi kiwakilishi cha kiima

Kiambishi kiwakilishi cha wakati

Yambwa

Mzizi - dhiki

Kauli ya kutendesha

Kiishio

**(g)** Tumia neno dhahiri kama: **(alama 3)**

**i.** Kitenzi______________________________________________________________

**ii.** Kivumishi____________________________________________________________

**iii.** Kielezi_______________________________________________________________

**(h)** Huku ukitoa mifano, eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili. **(alama 3)**

**(i)** Tofautisha mzizi na shina kwa mifano. **(alama 2)**

**(j)** Nyambua ziba katika kauli ya kutenduka kisha utungie sentensi. **(alama 2)**

**(k)** Bainisha hali zinazorejelewa katika sentensi hizi. **(alama 3)**

**(i)** Mwangeka hufika kituoni mapema.___________________________________________

**(ii)** Mgonjwa angetibiwa angepona._____________________________________________

**(ii)** Umekuwa nanasi, kutagia mibani?___________________________________________

**(l)** Andika katika udogo wingi. **(alama 2)**

Ugwe ulipitishwa juu ya ukuta uliomea uyoga na kufungiwa kwenye makuti.

**(m)** Onyesha kiarifu katika sentensi hii**.** **(alama 1)**

Kilimia kimechomoka angani.

**(n).** Changanua kwa kielelezo cha mstari. **(alama 3)**

Ndege aliruka angani ghafla.

**(o)** Ainisha Virai vinne katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Kicha cha funguo kilikuwa kimepotea jana nikicheza kandanda.

**(p)** Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya nukta mkato. **(alama 2)**

**(q)** Andika methali yenye maana sawa na jivu usilolilala usilipigie Jibwa. (**alama 1)**

**(r)** Andika upya sentensi ifuatayo ukianza kwa shamirisho kitondo. **(alama 2)**

Kaizari amewakatia ng'ombe majani kwa muundu.

**(s)** Damka ni kwa rauka, wakati ni kwa________________oa ni kwa taliki uza ni kwa_______

**(alama 2)**

**4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

Tamu sana! Very sweet! Very nutritious! Onja ujionee! Nunua. Nunua leo. Usikose mummy. Mchukulie mtoto. Fifty na Fifty! Hamsa. Fifty. Bure kwa bure! Bei ya starehe! Burudika.

**(i)** Tambua sajili hii. _______________________________________________ **(alama 1**

**ii)** Eleza sifa tisa za sajili hii kwa kurejelea kifungu. **(alama 9)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 7

**102/3**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 3

**MUDA: SAA 2½**

**JINA…………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………………  SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari ya utahini katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Jibu maswali manne pekee.*

***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima.*

***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki ; yaani,* ***Tamthilia, Hadithi Fupi, Riwaya na Ushairi.***

***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

***f)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**Kwa matumizi ya Mtahini Pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

## SEHEMU YA A. USHAIRI

**1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**.

Jiulize ni kwa nini, uanzapo kuongea Sana sana makundini, watu hukuondokea Ndugu ujitathmini, hakika umepotea
Sisi twakuombea, mwenye damu ya kunguni!

Mwenye damu ya kunguni, nayo lugha ya ajuza Wengi hawamtamani, maneno yake yaliza Yeye ana walakini, dosari kuliko pweza
Kama wewe umefunza, sote hutuona duni!

Sote hutuona duni, na hilo tumezowea Kazi zetu zote guni, yeye tu amebobea Umewachokoza mbuni, mateke anapokea Sisi twakuombea, upae hadi hewani!

Upae hadi hewani, ujione kama bingwa Mewashinda gazetini, wandishi kwako wapingwa Yeye kwetu mpinzani, metia mipaka tingwa Twakuombea mtafiti, hesabu hadi mizani!

Hesabu hadi mizani, utunge kwa kukosoa U hodari hesabuni, nasi tushakuzoea
We nduli kwa majirani, na waja mekutegea Kurekebisha hujui, ywatanika peupeni!

Ywatanika peupeni, ywajisifu mjuaji Amezidi zetu mboni, na amevijunjia mji Twamwachia waamuzi, kesi wasome majaji Sisi twakuombea, sirekebike kidogo!

**a)** Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili**(alama 6)**
**b)** Tambua miundo wa shairi hili**(alama 4)**
**c)** Tambua bahari ya shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa maneno.**(alama 2)**
**d)** Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari**(alama 4)**
**e)** Tambua aina tatu za takriri zinazojitokeza**(alama 3)**
**f)** Onyesha toni ya shairi hili**(alama 1)**

## SEHEMU YA B.
## TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA NA TIMOTHY AREGE

**2.** "…haikuwa mara moja mnavyofikiria. Ilianza pale chuoni. Wenzangu walinipa mvinyo kunirai kuonja ulevi."
**a)** Eleza maudhui manne yanayojidokeza katika dondoo hili.**(alama 4)**
**b)** Eleza athari za mhusika anayerejelewa kujitosa katika suala linaloredheshwa kwenye dondoo. **(alama 6)**
c Kwa kurejelewa mifano mitano katika tamthilia ya Bembea ya maisha, eleza tofauti iliyopo katika maisha ya ndoa ya zamani na sasa
**(alama 10)**

**AU**

**3. "** Maskini mke wangu ! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila

huruma. Awali niliona kama mchezo . Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imemsimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. Siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mfuriko msimu wa masika…Sasa nimekata shauri …Pombe! Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu . Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa"

**a)** Changanua mbinu **sita** za kimtindo zilizotumika katika kifungu hiki**.** **(alama 6)**

**b)** Taja na ueleze maudhui **manne** yanayojitokeza katika dondoo. **(alama 4)**

Jadili sababu kumi zilizompeleka mwandishi T. Arege kuandika Tamthilia hii. **(alama 10)**

**SEHEMU YA C . RIWAYA YA NGUU ZA JADI**

**4."**Nikupe ushauri dada.Kaa mbali naye kwani Yule ni moto wa kuotewa mbali.Ukimfuatafuata,anaweza kukutendea mambo mabaya"

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b)Tambua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

c)Andika sifa nne za "dada" anayetajwa na msemaji katika dondoo hili. **(alama 4)**

d)Jadili ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari. **(alama10)**

**AU**

**5.**

a)Chambua mtindo. **(al 8)**

Walitembea kuelekea mahali hapo kwa muda wa nusu saa.Mwishowe,waliona korongo kubwa.Ndanimwe,mlikuwa na walevi waliolala fofofo.Walikuwa wakipokezana mikoromo mizigo mizito iliyowashtua kina mama wale.Walijua lazima Mrima angekuwa hapo.Walipitapita huku wakiwakaguanyuso.Hakuna uso uliofanana na ule wa Mrima.Mangwasha akazidi kufadhaika.Alikuwa na uhakika kama mchana kwamba angemkuta mumewe mahali hapo.Wakaamua kwenda katika upande wa pili wa korongo hilo.Hapa pia palikuwa na walevi waliolewa chakari.Baadhi yao walikuwa wanavuta sigara.Wengine waliendelea kubugia pombe kutoka katika chupa walizobeba.Wengine tayari walikuwa wametekwa na usingizi.Walilala vinywa wazi bila kujali nzi waliong'ong'a nyuso zao.Lonare ndiye aliyemtambua Mrima.Alikuwa amelala kifudifudi,kaegemeza kichwa kwenye gogo.Lonare alimsukasuka ili aamke lakini wapi.

Mrima alikuwa akitabaradi kwenye ndoto zake,hana habari wala taarifa.Mkewe aliamua kumwita kwa nguvu huku akimfinya sikio.Mrima alihisi maumivu,akafungua jicho moja na kusema,"Nikilaala…shida i..iko wapi?Kwendeeni huko…ma…loofa nyie."Waliamua kumwinua.Walimbeba hobelahobela hadi kwenye gari.Alikuwa hatazamiki.Uchafu wa siku nyingi ulimfanya kunuka kama kisonzo.Nywele zilizosokotana.Maneno yalipiga manjano kutokana na ugaga uliokolea.Alivaa nguo bwaga mtwae tu.Nguo hizo zilicheua harufu mbaya mithili ya kicheche.Mangwasha chozi la huzuni lilimdondoka.Mrima alilalama huku akitoa matusi lakini hakuna aliyemsikiza.Lonare aliamua kumpeleka hospitali moja kwa moja.Hali yake ilihitaji matibabu ya dharura.Matibabu ya mwili na akili.

b)Jadili umuhimu wa mandhari ambamo kifungu hiki kimenukuliwa. **(al 12)**

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**D.W. Lutomia na Phibbian Muthama (wah.)**: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au 7*

*Msibu wa Kujitakia - D. W. Lutomia*

**6.** … kesho hoja zitakuwa msingi wa kupimia ubora wa wawaniaji uongozi.

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

b) Fafanua mbinu **nane** ambazo viongozi katika jamii hii wanatumia kupata uongozi. **(alama 8)**

c) Ukirejelea hadithi hii jadili jinsi wahusika mbalimbali wanavyojutia maamuzi yao. **(alama 8)**

**7.** a.Eleza nafasi ya vijana na wazee katika hadithi ya Mapambazuko ya machweo.**(alama 10)**

Nafasi ya vijana

b. Kwa hoja tatu, eleza umuhimu wa msimulizi katika kuendeleza hadithi ya mzimu wa kipwerere **(alama 10)**

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

***8.Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali yanayofuata.***

Msichana wa sura mzuri
Kitu gani kinakufanya usiolewe
Elimu unayo ya kutosha
Hata ngambo ukaenda ukarudi

Msichana wa urembo kama wewe
Uonyeshe mapenzi kwa vijana
Ukionyesha majivuno kwa vijana
Utazeeka ukiwa nyumbani kwenu

Ooh baby miaka yaenda mbio sana…

**a)** Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha. **(alama 2)**

**b)** Taja shughuli mbili za kijamii katika utungo huu. **(alama 2)**

**c)** Eleza toni ya utungo huu. **(alama 1)**

**d)** Wewe kama mwasilishaji wa fasihi simulizi, ni mbinu zipi ungetumia ili kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. **(alama 5)**

**e)** Maandishi ni mojawapo ya vifaa vya kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi. Tathmini udhaifu wa kutumia mbinu hii. **(alama 5)**

**f)** Eleza changamoto zozote nne zinazoweza kumkumba mtu ambaye angependa kuusanya data kuhusu kiperahiki.

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 8

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA**…………………………………………………………………………………………

**SHULE**……………………………………………… **SAHIHI**………………………

**NAMBARI YA USAJILI**…………………………… **MKONDO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika insha* ***mbil****i. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***

***b)*** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

***c)*** *Kila insha isipungue maneno* ***400.***

***d)*** *Kila insha ni alama* ***20.***

***e)*** *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

---

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**1. Insha ya lazima**

Umepata fursa ya kumhoji Waziri wa Ugatuzi nchini kuhusu mikakati ya kukabiliana na umaskini nchini. Andika mahojiano yenu.

**2.** Mitandao ya kijamii imeleta hasara nyingi kuliko faida. Jadili.

**3.** Andika kisa kinachodhihirisha maana ya methali:

Mti mkuu ukigwa, wana wa ndege huyumba.

**4.** Andika insha itakayomalizikia kwa maneno yafuatayo:

**…**Nilijitolea mhanga na msaada wangu ukazaa natija kwa wengi.

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 8

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA**……………………………………………………………………………………………

**SHULE**…………………………………………………  **SAHIHI**………………………

**NAMBARI YA USAJILI**……………………………… **MKONDO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

**1.** *Karatasi hii ina maswali manne (Ufahamu, Ufupisho, Lugha na Isimujamii)*

**2.** *Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa baada ya kila swali.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

***Soma kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Lugha inaweza kuelezwa kwa jumla kuwa ni mfumo wa kueleza chanzo au kiini cha mawasiliano na sote tunakubaliana kuwa matumizi yake yameanza tangu kuumbwa kwa binadamu kwani ni vigumu kukisia kuwepo kwa jamii ya watu bila lugha ya mawasiliano yoyote ile.

Katika taifa lolote,huwepo na lugha moja au hata zaidi ya moja ambayo huwa ndicho chombo zatika cha mawasiliano ya taifa katika nyanja za:elimu, maandishi, siasa na biashara.Kwa mfano mataifa ya Kanada hutumia lugha mbili kwa usawa kama lugha za taifa na za kikazi. Maana ya lugha ya taifa ni lugha moja ambayo huteuliwa kutumika katika shughuli zote za taifa hasa katika nchi yenye lugha nyingi za kikabila. Lugha ya taifa ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya taifa lolote lile.Lugha hii huwa ndiyo kiungo cha kueneza umoja na uelewano miongoni mwa jamii nyingi tofauti na huwa kama kitambulisho kwao kwa kuwa wao ni ndugu wa jamii moja kubwa, yaani taifa lao.

Kenya ni mfano mzuri wa taifa lenye lugha nyingi zinazozidi 40 za vikundi vidogo vidogo vya kikabila.Hapo kabla ya miaka mia moja hivi iliyopita kila kimojawapo cha vikundi hivi kilijitambulisha kama taifa huru.Baada ya kuja kwa serikali ya kikoloni na hasa baada ya Kenya kujinyakulia uhuru,haja ya kuunganisha raia wote chini ya taifa moja lenye uongozi na shabaha moja lilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana.Kwa hivyo utamaduni wa taifa la Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila,desturi,imani na itikadi tofauti. Utamaduni humaanisha jumla ya amali na tabia za watu wa jamii fulani. Amali hizi zinafungamanisha fikira, ustaarabu, mila, taasisi na sanaa za aina zote za jamii inayohusika. Ili kujieneza na kujiimarisha,taifa huhitaji chombo hicho kuwasiliana na kuwaunganisha watu wake wenye asili mbalimbali.Chombo hicho huwa ni lugha ambayo siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii bali pia ni njia muhimu sana ya kutawanyia na kustawishia ule utamaduni.

Katika taifa lenye lugha nyingi kama Kenya kwa mfano,lugha ya taifa inayozungumzwa na kueleweka na idadi kubwa ya raia ambayo imekiuka mipaka na tofauti za kikabila ni njia muhimu sana ya kueneza maongozi ya taifa, bendera ya taifa, ndicho kielelezo cha taifa lolote lile lililo huru. Lugha kama hiyo huvunja na hukomesha hisia za kibinafsi na kikabila na badala yake kuunda moyo wa uaminifu wa kitaifa.

Zaidi ya kuwa chombo cha mawasiliano, lugha ni kielelezo cha fikira na hisia za binadamu.Lugha ya watu fulani haituelezi tu ujuzi au maarifa yao bali pia mtazamo wao kimaisha, falsafa na mawazo yao. Kwa ufupi lugha hutufahamisha namna akili za watu waizungumzayo ile lugha zinavyofikiri na kutafanya maazimio.Lugha ni sehemu ya utamaduni wa taifa ilimozaliwa na lazima lugha hiyo ifunzwe katika muktadha wa maisha ya jamii ihusikayo.Utamaduni wa jamii havitenganiki na lugha yake.

## MASWALI

**(a)** Ni nini fasiri ya neno lugha? **(alama 2)**

**(b)** Tofautisha baina ya lugha ya taifa na lugha ya kikazi. **(alama 2)**

**(c)** Kwa nini lugha ya taifa huhitajika sana katika nchi kama Kenya? **(alama 2)**

**(d)** Taja kazi **tatu** kuu zinazotekelezwa na lugha ya taifa. **(alama 3)**

**(e)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na taarifa. **(alama 3)**

**(i)** Haiyamkiniki: ……………………………………………………………………
**(ii)** Amali na tabia za watu **:**………………………………………………………...........
**(iii)** Kielelezo**:**…….…………………………………………………………………
**(iv)** Muktadha wa maisha ya jamii: ……………………………………………………….

(f)Eleza majukumu mawili ya lugha kwa ujumla. **(alama 2)**

## 2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

***Soma kifungu kifuatasho kisha ujibu maswali.***

Kwa kawaida, binadamu huishi kwa kutangamana na binadamu wenzake. Katika kutangamana huku, watu huathiriwa kitabia, kifikira, kimavazi na kimaisha kwa jumla. Watu wote katika jamii wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa na wenzao wa umri mmoja. Hata hivyo, walio katika hatari ya kuathiriwa zaidi na mahirimu wao ni vijana. Hali hii ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika au shinikizo-marika. Vijana huaminiana na kuthaminiana sana. Kwa sababu hiyo, ni rahisi sana kuingizwa katika mitego na wenzao. Isiaminiwe kuwa vijana pekee ndio wanaoathiriwa na shinikizo-rika. La hasha! Watu wazima pia huwafuata wenzao mithili ya bendera kufuata upepo. Mwenzake akinunua gari, yeye pia hukimbilia mkopo kununua gari la sampuli iyo hiyo bila kuwazia kima cha kibindo chake.

Wataalamu wa saikolojia husema kuwa kukabiliana na tatizo la shinikizo-rika si rahisi kwa sababu shinikizo-rika huleta mtafaruku wa kinafsi akilini mwa anayeathiriwa. Nafsi moja humshawishi kufuata wenzake huku nyingine ikimnasihi kuandamana upekee au ubinafsi wake. Shinikizo-rika huathiri sana mahitaji ya kisingi ya binadamu. Ikumbukwe kuwa mahitaji haya ya kimsingi ni ya kila mwanadamu, nayo ni kama vile kupata lishe, hewa safi, kupenda na kupendwa miongoni mwa mengine. Kila mtu hutaka kujihusisha na kundi la watu ambao watamfanya kuhisi kuthaminiwa na kukubalika. Kutokana na haja ya kutaka kukubalika, anayetaka kutambuliwa huridhia matakwa ya wenzake bila hata kuyawazia.

Shinikizo-rika hujittokeza kwa sura nyingi. Mathalani, vijana huwafanya wenzao kuona kuwa wana hatia wasipoafiki kutekeleza kama wanavyoshinikizwa. Kauli kama vile ‘tulifikiri wewe ni mmoja wetu’ au ‘usiposhirikiana nasi utakuwa umetuvunja moyo’ hutamalaki. Wanaokataa kushinikizwa hubezwa na kufanyiwa stihizai na wenzao na hata kutengwa. Vitisho hutolewa, wakati mwingine, na anayeshinikiswa akidinda, mabavu hutumika.

Ni muhimu kwa watu, hasa vijana, kufahamu kuwa shinikizo-rika lipo na wanapokabiliwa na tatizo hilo, watambue kuwa wana haki ya kusimama kidete kutetea msimamo wao dhidi ya wenzao. Kumbuka, baridi huwazizima kondoo kwa namna tofauti.

Kama njia moja ya kukabiliana na shinikizo-rika, wanasaikolojia wanapendekeza watu kujiamini na kuelewa kwamba wana haki ya kuwa tofauti na kuwa na upekee wao. Mtu anapojiamini na kushikilia msimamo wake, anaweza kujiepusha na madhara yatokanayo na shinikizo-rika. Asiyejiamini huwa mwepesi sana wa kuingizwa katika lindi la mashaka na wenzake.

## MASWALI

**(a)** Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa **maneno (40)**.
**(alama 8, 1 ya utiririko)**

**Nakala chafu**

**Jibu**

**(b)** Fupisha mambo muhimu ambayo mwandishi amezingatia katika aya tatu za mwisho.
**(man 30)** **Jibu**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)

**(a)** Tofautisha kati ya: (i) / e / (ii) / u / **(alama 2)**

**(b)** Onyesha **muundo** wa **silabi** ya kwanza katika maneno yafuatayo: **(alama 2)**

**(i)** Nyakua
**(ii)** Chura

**(c)** Tunga sentensi kwa kutumia kibadala cha kiasi jumla. **(alama 2)**

**(d)** Changanua sentensi ifuatao kwa kutumia **jedwali**. **(alama 4)**
Mkongojo mrefu sana ulioletewa babu utauzwa na fundi mcheshi.

**(e)** Andika **kinyume** cha sentensi ifuatayo:
Mtoto msichana anathema dawa. **(alama 2)**

**(f)** Kanusha: **(alama 2)**
Nikimpiku masomoni nitatuzwa zawadi.

**(g)** Andika katika usemi halisi. **(alama 3)**
Chifu wetu alitwambia kuwa watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu.

**(h)** Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. **(alama 2)**
(i) (-la) (kauli tendeshea)
(ii) Toa (tendeka)

**(i)** Eleza matumizi ya alama zifuatazo za uakifishi. **(alama 2)**
(i) **!** **(ii)?**

**(j)** Bainisha mofimu **–Li-** katika tungo hili. **(alama 3)**
Alivyolikimbilia

**(k)** Tunga sentensi moja yenye shamirisho hizi. **(alama 3)**
**(i)** Kipozi (ii)Kitondo (iii)Ala

**(l)** Ainisha vishazi. **(alama 2)**
Mhamiaji haramu aliyeshikwa amefikishwa mahakamani.

**(m)** Andika katika wingi <u>karibu</u>. **(alama 2)**
Mtu yuyo huyo aliubeba mzigo uo huo licha ya kukanywa.

**(n)** Andika sentensi ifuatayo katika watati ujao timilifu. **(alama 2)**
Mbunge alitawazwa kabla ya mpinzani wake kufika.

**(o)** Andika kwa wastani. **(alama 1)**
Magoma haya yatachezwa wanjani.

**(p)** Taja na utoe mifano, matumizi <u>mawili</u> ya kiimbo. **(alama 4)**

**(q)** Eleza maana mbili za sentensi. **(alama 2)**
Nenda ukaniletee mbuzi.

## 4. SEHEMU YA D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

**(a)** Eleza mitazamo mine kuhusu chimbuko la Kiswahili. **(alama 4)**

**(b)** Eleza njia za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. **(alama 6)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 8

**102/3**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 3

**MUDA: SAA 2½**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………… SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
***c)*** *Swali la kwanza ni la* ***lazima****.*
***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**SEHEMU YA A: USHAIRI (ALAMA 20)**
**LAZIMA**

Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,
Ufyeke, upime na uweke nguzo,
Kisha paa uweke na ukandike,
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,
Nje na ndani ya nyumba watazunguka,
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,
Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,
Ukae nje nzima siku usubiri,
Wazima wamelala ukirudi usiku,
Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,
Na kisha wengine usiku mchana uwasake.
Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

**Maswali**

(i) Hili ni shairi la aina gani? **(alama 1)**
(ii) Eleza **muundo** wa shairi hili **(alama 3)**
iii) Eleza jinsi mshairi alivyoutumia **uhuru** wake katika utunzi wa shairi hili**.** **(alama 4)**
iv)Taja mbinu **mbili za lugha** alizotumia mshairi na uzitolee mifano. **(alama 4)**
v)Andika **ubeti wa tatu** kwa lugha nathari. **(alama 4)**
vi)Eleza **ujumbe** wa mshairi. **(alama 2)**
vii)Toa mfano mmoja wa mshororo **mshata.** **(alama 1)**
viii)Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? **(alama 1)**

**SEHEMU YA B:TAMTHILIA**
**BEMBEA YA MAISHA (TIMOTHY M. AREGE)**

Jibu swali la 2 au 3

**2.**'' Lakini ndiyo tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama...kama…kama vile tambara bovu.''

a. i)Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. **(Alama 4 )**
ii)Tambua mbinu **mbili** za kimtindo katika dondoo. **(Alama 2)**
b) Fafanua **umuhimu wa msemaji** katika kujenga ploti. **(Alama 4)**

c) **Utamanduni** huthaminiwa sana na jamii ya tamthilia ya Bembea ya Maisha. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutoa mifano **kumi** mwafaka tamthiliani. **(alama 10)**

3.Beni:Afadhali hao.Mjukuu wangu hatofautishi kondoo,mbuzi na mbwa.Wote hao kwake yeye ni mbwa!(*wanacheka wote)*

Yona: Inachekesha.

***Swali***

Mazungumzo haya kati ya Beni na Yona yanabainisha tofauti iliopo kati ya suala la *usasa na ukale*. Kwa kutoa mifano **kumi** inayoonyesha usasa na **kumi** inayoonyesha ukale,linganua masuala haya. **(alama 20)**

**SEHEMU YA C: RIWAYA**

**NGUU ZA JADI:*CLARA MOMANYI***

*Jibu swali la 4 au 5*

4."Naweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake."

(a)Weka dondoo hili katika **muktadha** wake. **(alama 4)**

(b)Tambua **maudhui** katika dondoo hili. **(alama 4)**

(c)Kwa kutoa mifano **kumi na miwili** mwafaka kutoka riwayani,onyesha jinsi maudhui uliyotambua hapo juu(4b) yalivyoshughulikiwa na mwandishi**.** **(alama 12)**

5. **Tamaa na ubinafsi** ni baadhi ya masuala makuu yaliyoshughulikiwa kwa mapana na marefu na *Clara Momanyi* katika riwaya yake ya *Nguu za Jadi*. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani thibitisha ukweli wa kauli hii. **(alama 20)**

**SEHEMU YA D :HADITHI FUPI**

***MAPAMBAZUKO YA MACHWEONA HADITHI NYINGINE***

*Jibu swali la 6 au 7*

**WINNIE NYARURI OGENCHE:SABINA**

6.Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.

a)Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. **(alama 6)**

b)Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. **(alama 4)**

c)Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. **(alama 10)**

**YUSSUF SHOKA HAMAD:** ***Mzimu wa Kipwerere***

**7.“…**Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama.”

(a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(Alama 4)**

(b)Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(Alama 4)**

(c)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. **(Alama 2)**

(d)Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. (alama 10)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

***Swali la nane***

8. a) Ulumbi ni nini? **(alama 2)**

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii?. **(alama 6)**

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. **(alama 6)**

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. **(alama 6)**

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 9

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1**

**MUDA: SAA 1¾**

JINA……………………………………………………………………………………

SHULE……………………………………………… SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**102/1**
**KISWAHIL**
**KARATASI YA KWANZA**
**MUDA: SAA 1 ¾**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

***a)*** *Andika jina lako, nambari ya usajili na tarehe katika karatasi ya majibu.*
***b)*** *Karatasi hii ina maswali manne.*
***c)*** *Jibu maswali mawili pekee. Kila swali lina alama ishirini.*
***d)*** *Swali la kwanza ni la lazima.*
***e)*** *Chagua swali lingine lolote moja kutoka yale matatu yaliyosalia.*
***f)*** *Majibu yote yaandikwe katika karatasi ya majibu uliyopewa.*

***Sehemu hii imehifadhiwa kwa matumizi ya mtahini pekee.***

| SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 |
|---|---|---|---|---|
| UPEO | 20 | 20 | 20 | 20 |
| ALAMA | | | | |

| UPEO | 40 |
|---|---|
| ALAMA ZA MTAHINIWA | |

**MASWALI**

**1.** Wewe ni mwanahabari mtajika nchini. Umepata fursa ya kumhoji Waziri wa Afya kuhusu njia mbalimbali za kukabiliana na maradhi yasiyo na tiba. Andika mahojiano yenu.

**2.** Eleza njia mbalimbali zinazofaa kuchukuliwa na serikali katika kukabiliana na migogoro ya kifamilia nchini.

**3.** Andika insha inayoafiki methali**: Asiyejua faida ya mwangaza aingie gizani.**

**4.** Tunga kisa kitakachoanza kwa maneno yafuatayo:

Hospitali ilionekana kumetameta kwa wingi wa watu**...**

KCSE 26

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 9

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

JINA………………………………………………………………………………………

SHULE………………………………………………    SAHIHI………………………

NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO:**

(i) *Andika jina lako, nambari yako ya usajili na darasa katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

(ii) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

(iii) *Jibu maswali yote.*

(iv) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

(v) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

***Kwa matumizi ya mtahini pekee.***

| | Swali | Upeo | Tuzo |
|---|---|---|---|
| A | Ufahamu | 15 | |
| B | Ufupisho | 15 | |
| C | Matumizi ya lugha | 40 | |
| D | Isimu jamii | 10 | |
| | JUMLA | 80 | |

**SEHEMU A.(Alama 15)**

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali*

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za kulitandarukia tatizo ambalo linakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaokabili mataifa yanayoendelea, unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale kama vile marekani, nchi za ulaya na ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umaskini huu ni anuwai mathalan, ufisadi uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na mali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini, ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelea kuwa umaskini unaothiri nchi fulani una athari pana sana. Uvunjifu unaotokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambako matendo mabaya huchipuka. Raia maskini huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifo ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburia madeni ya mataifa yanayoendelea kama kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umaskini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tagemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa ufupi ,maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisia wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

**Maswali:**

**a)** Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea**?** **(alama 4)**

**b)** Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea**.** **(alama 2)**

**c)** Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la umaskini**?** **(alama 4)**

**d)** Mfumo wa soko huru una madhara gani kwa mataifa **machanga** **(alama 2)**

**e)** Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: **(alama 3)**

I. Kulitandarukia……………………………………………………………………………………

II. Kuatika……………………………………………………………………………………………

III. Kuyaburia madeni ---------------------------------------------------------------------

**SEHEMU YA B :UFUPISHO.(alama 15).**

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata*

Kadiri jamii mbalimbali zinavyotagusana, ndivyo lugha zinazozungumzwa na jamii hizi nazo zinavyoingiliana na kuathiriana . Mojawapo ya athari hizi ni ukopaji wa msamiati kutoka kwa lugha jirani na kuutumia kuelezea dhana mpya zinazoingia katika utamaduni wao kupitia kwa mitagusano ya kijamii.

Lugha ya Kiingereza kwa mfano, imekopa kutoka lugha nyingine kama vile Kifaransa na Kilatini. Mathalani, istilahi nyingi za kisheria zimekopwa kutoka lugha ya kifaransa. Aidha,Kiingereza kimekopa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili kama vile mwalimu, jiko, mandazi, panga , buibui, ngoma na hata wananchi, sasa yameingia katika kamusi za Kiingereza, kumaanisha kuwa yamekubaliwa kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiingereza.

Kiswahili nacho kimeathiriwa na lugha nyingine. Kimekopa msamiati wa Kiingereza na hata Kiarabu. Katika tungo nyingi za kishairi, kwa mfano, utenzi wa Mwanakupona utapata msamiati wa Kiarabu uliotoholewa. Lugha nyingine ambazo zimeathiri Kiswahili ni pamoja na Kijerumani ambako msamiati kama vile ‘shule’ ulikopwa na kutoholewa kutokana na neno schule. msamiati kama vile ‘leso’, ‘karata’ na ‘mvinyo’ yamekopwa kutoka lugha ya Kireno, huku majina ‘balozi’ na ‘bahasha’ yakikopwa kutoka Kituruki.

Pamoja na ukopaji wa vipengele vya lugha, mtagusano wa lugha una athari nyingine. Lugha zinapokuja pamoja, mazingira ya wingi-lugha hazuka. Baadhi ya watu hujifunza zaidi ya lugha moja. Mtu anayeweza kuzungumza zaidi ya lugha moja anaweza kujieleza kwa urahisi kwa kuchanganya msamiati wa lugha tofauti. Aidha, anaweza kubadilisha msimbo kulingaa na matilaba yake. Ikiwa anataka kukubalika na jamii-lugha anayotagusana nayo,anatumia lugha ya jamii hiyo ili kujinasibisha nayo. Wazungumzaji hupata visawe vya maneno kuelezea dhana zile zile, hivyo kuboresha mitindio yao ya mawasiliano

Kadhalika, kutagusana kwa lugha kunaweza kusababisha kubuniwa kwa lugha ngeni ambayo inarahisisha mawasiliano. Wakati mwingine, watu wanaozungumza lugha tofauti wanapokutana, hubuni mfumo sahili wa lugha ili kufanikisha mawasiliano. Pijini ni mfano wa lugha iliyobuniwa kwa njia hii. Pijini huchota msamiati kutoka lugha zilizotagusana. Sheng ni mfano mwingine wa lugha ambayo ilibuniwa kutokana na kutagusana kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kiasili na kiingereza.

Japokuwa kuna faida nyingi za wingi-lugha, hasara pia zipo. Mazingira ya wingi-lugha huwapa wazungumzaji fursa ya kuchagua lugha wanayotaka kuwasiliana kwayo. Katika hali hii, lugha yenye ushawishi mkubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa ndiyo inayopendelewa zaidi. Wingi-lugha unaweza kusababisha kukweza kwa lugha moja na kudunishwa kwa lugha nyingine, mathalini. Kuwepo kwa lugha nyingi nchini kulizua haja ya kukwezwa kwa lugha ya Kiswahili huku lugha nyingine za kiasili zikipuuzwa.

Lugha hukua kwa kutumiwa. Lugha isipozungumziwa kwa muda mrefu, watu hupoteza umilisi ambao huifanya kuwa vigumu kuirithisha kwa vizazi. Lugha inaweza pia kukosa wazungumzaji ikiwa wale wanaozungumza ni wachache au ikaathiriwa na mtagusano na lugha nyingine iliyo na wachache au ikaathirisha na mtagusano na lugha nyingine iliyo na wazungumzaji wengi.

Katika hali kama hii, lugha hiyo hukubaliwa na tisho la kudidimia au hata kufa. Ikiwa jamii itakosa kudhibiti sera za matumizi ya lugha yake, baadhi ya lugha zitafifia au zitakufa na kusahaulika kabisa.

**a).** Bila kupoteza maana,fupisha aya za kwanza tatu(maneno 50)alama 8,2mtiririko)

**MATAYARISHO**

JIBU

**b)** .Kwa mujibu wa taarifa hii,mtagusano wa lugha una athari gani?(maneno 30) alama 7,1mtiririko)

**MATAYARISHO**

**JIBU**

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**a)** Andika neno lenye muundo ufuatao wa **sauti** **(alama 2)**

**Kipua cha kaakaa laini, irabu ya kati tandazwa, kipasuo sighuna cha ufizi, irabu ya chini.**

**b)** Taja aina mbili kuu za ala za sauti kisha utoe mfano mmoja mmoja **(alama 2).**

**c)** Tumia kivumishi kionyeshi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya I-ZI, Kisha utunge sentensi katika ukubwa –wingi. **(alama 2).**

**d)** Yakinisha sentesi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi. **(alama 1)**

Msomi hakutuzwa siku hiyo

**e)** Tumia mzizi –w- katika sentensi **kama** **(alama 2)**

i)kitenzi kisaidizi

**ii)**kitenzi kishirikishi

**f)** Ainisha viambishi kwa kurejelea majukumu ya kisarufi katika neno hili **(alama 3)**

**Alijipelekea**

**g)** Maneno yaliyopigiwa mstari yametumikaje? (**alama 1)**

Pahali <u>pema</u> pako si <u>pema </u>pa mwenzako.

**h)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi **(alama3)**

**Mlango umevunjwa na fundi aliyeujenga**.

**i)** Onyesha matumizi ya chagizo ya mfanano katika **sentensi** **(alama 2)**

**j)** Andika katika usemi wa taarifa**.** **(alama 3)**

“Hicho kijicho cha paka cheupe leo marufuku kwangu”alisema mzee Kambumbu.

**k)** Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu lake. **(alama 2)**

**Pika ugali kwa kuku kila Jumamosi ukitumia gesi.**

**l)** Panda ni kuatika mbegu ardhini au kuparaga mti. Andika maana nyingine mbili. **(alama 2)**

**m)** Tunga sentensi moja ukitumia **kihisishi cha bezo** **( alama 1)**

**n)** Tunga sentensi na ubainishe **kijalizo** **(alama1)**

**o)** Tunga sentensi yenye muundo wa: **(alama 3)**

**Kiima, kiarifa, yambwa tendwa, yambwa tendewa na yambwa ala.**

**p)** Eleza maana ya msemo ufuatayo **(alama1)**

**Piga unyende**

**q)** Eleza tofauti iliyopo kati ya jozi hii ya sentensi**.** **( alama 1)**

i)Kerubo alinikimbilia.

ii)Kerubo alinikimbia.

**r)** Weka nomino ifuatayo katika ngeli yake **(alama 1)**

**Mbalungi**

**s)** Tumia kiungo 'na' katika sentensi kuonyesha **(alama1)**

i)ufupisho wa nafsi ya kwanza umoja fulani

ii)kihusishi kuonyesha aliyetenda jambo fulani.

**t)** Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari: **(alama2)**

Ubora wa kazi zao ulifichika baada ya kuanzishwa kwa mradi ule.

**u)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao**.** **(alama 2)**

**KN(N) + KT (T+E) + U+KN(N)+KT(T+E)**

**v)** Eleza matumizi ya kiambishi 'ki'katika sentensi hii. **(alama2)**

**Njia hii haipitiki**

**ISIMUJAMII(ALAMA 10).**

**a)**Kwa kutumia hoja sita zilizofafanuliwa vyema, jadili tofauti zipatikanazo kati ya sajili ya maabadini na ile ya mahirimu. **(alama 6)**

**b)**Sajili za lugha huwa na umuhimu anuwai.Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja nne**.** **(alama 4)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 9

**102/3**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 3

**MUDA: SAA 2½**

**JINA**……………………………………………………………………………………

**SHULE**………………………………………………… **SAHIHI**………………………

**NAMBARI YA USAJILI**……………………………… **MKONDO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Jibu maswali manne **pekee**.*
***b)*** *Swali la **kwanza** ni la **lazima***
***c)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya Hadithi fupi,Tamthilia na Ushairi.*
***d)*** *Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.*
***e)*** *Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

## SEHEMU YA A : RIWAYA

***CLARA MOMANYI: Nguu Za Jadi***

***LAZIMA***

**1.** "Waite. Unadhani mapenzi yanaogopa polisi"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

(b) Fafanua sifa **sita** za msemewa **(alama 6)**

(c) Kwa kutoa mifano taja mbinu **tatu** za kimtindo katika dondoo hili **(alama 3)**

(d) Msemewa na wenzake ni adui wa wananchi wa Matuo. Fafanua ukweli kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Nguu Za Jadi **(alama 7)**

## SEHEMU YA B: TAMTHILIA

***Timothy Arege: Bembea ya Maisha***

***Jibu swali la 2 au la 3***

**2.** (a) "Maradhi! Madhila yake hayasemeki. Yakimla mtu humthakilisha. Humwacha hoi,hana mbele wala nyuma."

i. Eleza muktadha wa dondoo **hili** **(alama 4)**

ii. Fafanua toni katika dondoo **hili** **(alama 1)**

iii. Eleza sifa nne za msemaji **(alama 4)**

iv. Taja na ufafanue mbinu za kimtindo katika dondoo hili **(alama 3)**

(b) Changanua mtindo **(alama 8)**

"Bunju ni mmoja wenu. Nyote ni wanangu." Hayo ni maneno ya mama. Wakati huo sikuona. Sasa naona. Wanasema mwenye macho haambiwi tazama. Kweli iliyoje! Japo hutokea wakati tukalalamika,ninafikiri Bunju ni zawadi nzuri kwetu. Leo tungekuwa wapi bila Bunju? Maji yangezidi unga. Usingepikika,usingelika.(kimya) Hebu fikiri! Umepata ajali mbaya. Inakuacha mahututi. Anapita mtu katika gari lake. Kwa imani anaguswa. Anakufanyia mpango wa Flying Doctors;ndege inafika na kukupeleka hospitali. Mwenyewe huyo analipia kila kitu!mtu huyo atakosaje kuwa zawadi kwako?

3. "Mama sijaona baba akipika hivi karibuni."

Kwa kurejelea nukuu hii fafanua usasa na utamaduni vilivyosawiriwa katika tamthilia ya Bembea ya **Maisha** **(Alama 20)**

## *SEHEMU YA C: HADITHI FUPI*

***Rachel Wangari: Fadhila za Punda***

***Winnie Nyaruri Ogenche: Sabina***

***Jibu swali la 4 au la 5***

**4.** ***Racheal Wangare:Fadhila za Punda***

"Rudi, nyumbani mwanamke wewe! Nitakuja jioni tuyamalize haya."

a) **(i)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

(ii) Fafanua hulka ya msemaji wa kauli hii **(alama 4)**

iii) Huku ukizingatia hadithi hii, jadili maudhui ya mabadiliko yanavyojitokeza katika hadithi **(alama 7)**

b) *Changanua mtindo katika dondoo hili* **(alama 5)**

Aligutuka kutoka kwenye usingizi wa mang'amung'amu,roho mkononi,pumzi zikimkwenda mbio. Hakujua kilichomwamsha,hivyo alitega sikio ndi! Isije akawa mwenye nyumba akaja na yeye mpangaji akachelewa kumfungulia mlango;itakuwa balaa bin beluwa. Ndio maana amelala pale juu ya kochi ili akiingia tu,hata kabla ya kubisha mlango,awe tayari kuufungua. Hilo litampa usalama,japo kwa muda tu. Baada ya kusikiliza kwa makini na kuchungulia nje,hakumwona aliyemtarajia.Asaa akaamua asifike leo.Lakini hilo halikumpunguzia wasiwasi mwenzetu,maanake kesho pia ni siku.Atakuja tu,labda ghamidha itakuwa imezidi,imefura kama hamri lililotiwa hamira.Matokeo yake aliyajua.Si bughudha hizo,nyanyaso moto mmoja.Naye yuko pale tu,subira kifuani,dua mdomoni. Walisema mvumilivu hula mbivu ila yeye hakujua stahamala yake ingempeleka wapi!

**AU**

**5. *Winnie Nyaruri Ogenche; Sabina***

"Ninaomba wazazi wenzangu muwape watoto wa kike elimu badala ya kuwaoza mapema. Hongera, mwanangu kwa kupata alama mia nne arubaini na saba"

a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika **(alama 5)**

b) Tambua mbinu ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili **(alama 1)**

c) Fafanua jinsi mbinu yenyewe ilivyotumika ili kufanikisha utunzi wa hadithi **(alama 6)**

d) Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi **(alama 8)**

***SEHEMU YA D: USHAIRI***

***Jibu swali la 6 au la 7***

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali
Ubavuni umuweke, umtowe kule mbali
Maskanini afike, umtindie fahali
Utamu anufaike, sima, bada au wali
Hatimaye ateuke, kwa viliwa vya samli
Mwanadamu simwamini, afadhali mnyama lumbwi.

Mwanadamu umjenge, awe mwenye kutajika
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka
Nao mkono umuunge, vyake viwe vyaungika
Dhorubani umkinge, asipate kudhurika
Mara atakusahau, wema wako kafukia

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie
Amani yako umpeo, fanaka uirajue

Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue
Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue
Ndio wake mwelekeo, yuauma avuvie
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililo jema
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema
Viteko siwe akali, kumbizo zikaterema
Binadamu takudhili, dhili zako kazitema
Licha ya zote jamili, mwanadamu si muema
Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama

**Maswali**

a) Shairi hili ni la aina gani? Fafanua jibu lako. **(alama 2)**

b) Eleza usaliti unaoendelezwa na mwanadamu kwa mujibu wa shairi hili. **(alama 4)**

c) Tia shairi hili katika bahari tatu tofauti kwa kuzingatia; **(alama 3)**

**i.** Mpangilio wa maneno
**ii.** Mpangilio wa vina
**iii.** Mgao wa mishororo

d) Eleza muundo wa shairi hili. **(alama 4)**

e) Bainisha toni ya shairi hili. **(alama 1)**

f) Eleza mbinu mbili ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa kwanza. **(alama 2)**

g) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama 4)**

**7.** Nimeyaandika maneno haya
Kwa niaba ya:
Mamilioni wasio malazi
Wabebao vifurushi vilivyo wazi
Wazungukao barabarani bila mavazi
... milki yao ya maisha.
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki
Wiki baada ya wiki
leo sumu au spaki
leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
wale mayatima wa maskini
wazungukao mapipani
kila pembe mjini

kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza
walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
polepole wakijiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana watazama
wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
Kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
bila ya mtu kuona
kama kwamba sote tu vipofu,

Na kwa niaba yetu sote;
Tuliofungwa vifungoni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni, machoni
Tuliotiliwa sumu, malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini
ili 'maendeleo'
yaendelee kwenda njiani
huku yakitema machicha ya roho zetu.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Fafanua . **(alama 2)**
b) Bainisha toni ya shairi hili . **(alama 2)**
c) Tambua aina tatu za urudiaji zinazojitokeza katika shairi. **(alama 3)**
d) Huku ukitoa mifano eleza namna mtunzi alivyotimiza arudhi za kishairi. **(alama 3)**
e) Eleza matumizi ya**.** **(alama 3)**
i. Mistari mishata
ii. Mistari kifu
iii. Tasfida
f) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. **(alama 2)**
g) Tambua aina za taswira katika shairi hili. **(alama 2)**
h) Mshairi anazungumza kwa niaba ya watu mbalimbali. Jadili. **(alama 4)**

***SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI***

*(a) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

Hadithi ya Jabari inasimuliwa na jamii nyingi. Jabari alizaliwa kashika mkuki mkononi. Mawio ambayo kilio chake,ambacho kwa kweli kilikuwa mngurumo,kilipasua anga,nyota kubwa ilianguka kutoka mbinguni.ulimwengu mzima ulitetemeka kwa kutwaa giza.

Hata kabla mama mtu hajampa ziwa,Jabari alikuwa amevuvumka na kuwa ghulamu wa miraba minne. Haikuchukua muda,hata vita kati ya jamii ya Sule na Suna vikaanza;kikosi cha Sule cha wapiganaji mia moja kikawajia vijana wa Suna kwa sime na nyuta. Jabari aliwakabili kwa konde moja pekee,akakirambisha dongo kita kizima.

i. Bainisha kipera cha utungo huu **(alama 1)**

ii. Toa sababu mbili kuthibitisha jibu lako **(alama 2)**

iii. Eleza manufaa matano ambayo jamii itapata kwa kurithisha kipera hiki kwa vizazi vijavyo **(alama 5)**

*(b) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

Ndimi Mwimo mdumishaji ukoo
Ndimi ndovu mtetemesha ardhi
Aliyepigana vita,ukoo kuauni
Ziliporindima zangu nyayo
Adui alinywea,mafahali na mitamba akatukabidhi
Kwenye msitu sikuwa na kifani
Paa na hata visungura
Vilijikabidhi kwangu
Kwa kuinusa tu mata
Nani aliyewahi
Ngomani kunipiku? Makoo hawakunisifu,wakalilia nikaha?
Kwenye nyanja za michuano
Nani angethubutu,ndaro kunipigia?
Sikuwabwaga chini, kwa yangu maozi,hata kabla hatujavaana?

**i.** Hii ni sifo gani? **(alama 1)**

**ii.** Bainisha shughuli **moja** ya kiuchumi na **moja** ya kijamii zinazoendelezwa na jamii inayosawiriwa na utungo **huu** **(alama 2)**

**iii.** Eleza mambo **matano** ambayo yanaweza kuzingatiwa ili kufanikisha uwasilishaji wa uungo huu **(alama 5)**

(c) Eleza faida **nne** za matumizi ya nyimbo katika uwasilishaji wa ngano **( alama 4)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 10

**102/1**

# KISWAHILI

## KARATASI YA 1

**MUDA: SAA 1¾**

**JINA………………………………………………………………………………………**

**SHULE…………………………………………………     SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI……………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

h) *Andika jina lako na nambari ya usajili kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
i) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
j) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
k) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
l) *Kila insha isipungue maneno **400**.*
m) *Kila insha ina alama **20.***
n) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.***
o) *Insha zote sharti ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa kwenye kijitabu hiki cha maswali.*

**<u>Kwa matumizi ya mtahini pekee</u>**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| **Jumla** | **40** | |

## MASWALI

**1.** Wewe ni mtangazaji wa kituo cha utangazaji cha Uzalendo. Studioni umetembelewa na mwanamke mtetezi wa haki za wanawake kuzungumzia namna mwanamke ametelekezwa katika jamii ya sasa. Andika mahojiano kuhusu mchakato huo. **(Alama 20)**

**2.** Kuna njia anuai zinazoweza kutumiwa kulitandarukia tatizo la ajira nchini. Tetea. **(Alama 20)**

**3.** Andika kisa kinachoafiki methali**; Mgagaa na upwa hali wali mkavu.** **(Alama 20)**

**4.** Tunga kisa kitakacho kamilika kwa kauli ifuatayo;

**…**niliduwaa, nikasimama kisha nikaangalia nyuma huku machozi yakinitoka. Nilikumbuka wosia wa walimu na wazazi wangu, lakini kitumbua changu kilikuwa kimeingia mchanga**(Alama 20)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 10

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA**……………………………………………………………………………………

**SHULE**…………………………………………… **SAHIHI**………………………

**NAMBARI YA USAJILI**…………………………… **MKONDO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**Maagizo kwa watahiniwa**

1. *Andika jina lako, nambari, na darasa lako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
2. *Andika tarehe ya mtihani na utie sahihi yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
3. *Jibu maswali* ***yote.***
4. *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa baada ya kila swali katika kijitabu hiki cha maswali.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | 80 | |

**1. UFAHAMU (Alama 15)**

***Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Yasemekana kuwa Shungwaya ndicho kitovu cha watu waishio Giriama katika janibu za pwani ya Kenya na wanaojulikana kwa jumla kana Wamijikenda. Yaaminika kuwa bado wakiwa Shugwaya, walimuua Mgalla mmoja mwenyeji wa Shungwaya na kitendo hicho kiliamsha hasira kali za Wagalla, hata ikawawia vigumu Wamijikenda kuishi kwa usalama pamoja na ndugu zao hao.

Hata hivyo, Wamijikenda hawakugura mara moja wala wote kwa pamoja bali walihama katika vipindi tofuati na katika makundi madogomadogo. Kila kundi lililofika Giriama lilijenga 'kaya' au mji wake. Kwa jumla, walihama kwa makundi tisa.

Vile vile, Wamijikenda walihama na fingo yao ambayo ilifukiwa na viongozi wao katikati ya kaya zao, palipokuwa na msitu mdogo. Hakuna ajuaye hasa mahali ilipofukiwa ila wazee hao waliopenda kufanyia baraza mahali hapo.

Mnamo mwaka wa 1870, mzee Menza na mkewe walibarikiwa kufungua kizazi kwa kupata mtoto wa kike waliyemwita Mekatilili. Walimlea vizuri na alipoanza kuzungumza, alionyesha dalili za kuwa na kipawa cha pekee. Kwanza, alipenda kujua kila kitu kilichoihusu jamii yake na pili alichukizwa sana na kiumbe aliyemdhulumu kiumbe mwenzake. Kwa mfano, aliwaonea vipepeo imani walipoliwa na ndege. Tena alizipenda sana mila na desturi za watu wa jamii yake – Wamijikenda.

Siku moja, baada ya Mekatilili kufikia utu uzima, mama yake alimwita chemba akamwambia, "Mwanangu sasa umeshabalehe, nami ningependa kuwaona wajukuu wangu kabla sijawafuata wazee waliotangulia. Waonaje tukikuoza? Mimi na baba yako tumepata mume ambaye ni kufu yako kabisa."

"Ninaelewa, maana hizi ni desturi zetu, lakini ningefurahi zaidi kama mngeniruhusu nijichagulie mume ninayempenda." Binti alimjibu mamaye.

"Mnazi na uwe mrefu, huyumba kufuata upepo." Mama akajibu. Tangu hapo binti akawa hana la kujibu ila kukubali.

Siku ya harusi, watu wengi walihudhuria na wakastarehe kwa tembo la mnazi ambalo lilikuwa limetengenezewa kwa wingi. Jioni hiyo, mekatilili alichukuliwa kwa mumewe Masendeni, karibu na mto Sabaki. Ikawa hangeonana na wazazi wake kila siku kama ingalivyokuwa mapenzi yake. Wakati huu kote nchini Kenya kulikuwa kumejaa wageni, wengi wao wakiwa walowezi na watawala wa kibeberu. Walikuwa wameanzisha mashamba ya mikonge, kahawa na chai. Walihitaji watu wa kupalilia mashamba yao hayo. Hata hivyo Waafrika hawakuwa na haja ya kulima wala pesa. Hata walipolima, ni kwa minajili ya kubadilishana mazao na kula.Iliwabidi Wazungu kutumia mizungu ili kuwashurutisha Waafrika kuwalimia. Baadhi ya mikakati waliyobuni ni kuwateka nyara watu barobaro na kutoza kodi. Ni katika harakati kama hizo ambapo mumewe Mekatilili alitekwa, asirudi tena kwake. Wakati uo huo, wazazi wa Mekatilili waliaga dunia.

Mambo haya yalimpa mekatilili msukumo. Baada ya muda wa kuomboleza kuisha, alijiunga na wazee wapigania ukombozi, mmoja wao akiwa Wanje, kakaye mumewe. Aliwaunganisha

wanawake na kuwahimiza wasiige mila na desturi za kizungu. Aliwahutubia wanaume na kuwakumbusha kuwa ilikuwa lazima wailinde nchi yao. Siku moja alishikwa kwa kuwalisha watu kiapo. Alipelekwa bara, Kisii, mbali kabisa na kwao, Masharibi mwa Kenya na akatiwa kizuizini pamoja na Wanje. Hata hivyo, walifaulu kutoroka na kwa muda wa siku ayami walipitia kwenye mabonde na milima, misitu na nyika hadi wakarudi Giriama.

Mabeberu walikasirika sana. Hata hivyo, walikuwa wamechelewa. Katika safari yao kurudi Giriama, walifaulu kuhubiria wengi dhidi ya mgeni. Vita vya ukombozi vilikuwa vimeshika.

**Maswali**

**1.** Ni kwa nini Wagiriama wanajulikana kama Wamijikenda? **(al.1)**

**2.** Ni maafa gani yaliyompata Mekatilili katika maisha yake? **(al.4)**

**3.** Ni hali gani inayotawala katika makala haya. **(al.2)**

**4.** Taja masuala ya kijinsia yanayojitokeza katika Makala haya. **(al.2)**

**5.** Wazungu walitumia mbinu gani ili kuwashurutisha watu kuwafanyia kazi mashambani mwao. **(al.2)**

**6.** Andika maneno mengine yeney maana sawa na;

i) Kugura……………………………………………………….…………………**(al.1)**

ii) Kubalehe…………………………………………………………………..**(al.1)**

**7.** Eleza maana ya;

i) Mnazi na uwe mrefu huyumba kufuata upepo

……………………………………………………………………………………**(al.1)**

ii) Kitovu cha watu waishio Giriama

…………………………………………………………………………..…**(al.1)**

**2. UFUPISHO (Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Kiswahili tunasema ni lugha yetu kwa sababu ndiyo lugha ya Kiafrika inayoongewa katika nchi nyingi Barani Afrika. Ni lugha yetu kwa sababu ni lugha asilia mojawapo za Afrika. Siyo lugha iliyoletwa na watu wa nchi za nje kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Uzuri wa Kiswahili sasa ni kuwa kimeenea kote Afrika Mashariki na Kati.

Wenyeji asilia waliokuwa wakiongea lugha hii tangu awali ni Waswahili. Waswahili hawa hata leo wako na wanaendelea kuitumia lugha hii kama lugha yao ya mama, kama vile Wakikuyu watumiavyo Kikikuyu, Wakamba, Kikamba na Wadigo lugha ya Kidigo. Makao yao Waswahili tangu jadi yanapatikana kaunti ya Pwani. Makao yao yameanzia upande wa Kaskazini Mashariki ya Kenya , na wanapakana na nchi ya Somalia huko. Wameenea katika upwa huo wa Pwani, ikiwamo Lamu, Malindi, Mombasa, Pemba, Unguja, Visiwa vya Ngazija na kuendelea.

Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi kulingana na sehemu wanamoishi. Kwa mfano, Waswahili wa Lamu huongea lahaja ya Kiswahili inayoitwa Kiamu. Waswahili wa Mombasa huongea lahaja ya Kimvita. Pemba wanaongea Kipemba, Ngazija lahaja ya Kingazija, Unguja lahaja ya Kiunguja na kadhalika. Kutokana na lahaja hizi na nyinginezo za Kiswahili ambazo

hazikutajwa hapo, wataalamu wa lugha walitokea na Kiswahili sanifu. Hiki Kiswahili sanifu ndicho kitumiwacho katika mafunzo ya shule, uandishi wa vitabu na mawasiliano ya kiserikali na kibiashara.

Nchini Kenya, kwa muda mrefu Kiswahili hakikuthaminiwa kama Lugha ya Kiingereza. Sababu mojawapo ni kuwa Kiswahili hakikufanywa somo la lazima katika rasimu za shule, wala kutahiniwa katika shule za msingi. Hata katika shule za upili, katika kufunzwa na kutahiniwa hakikupewa umuhimu wowote. Kwa ajili hii wanafunzi wengi waliacha kujifunza Kiswahili kama somo. Hali hiyo ilifanya Kiswahili kuonekana kama lugha inayoongewa na wale watu wasio na kisomo ama elimu nyingi. Kwa ajili ya fikira hizi, watu wengi wamekuwa wakikichukia, kukidunisha na kujaribu kuongea Kiingereza kila nafasi inapojitokeza.

Miaka michache iliyopita, Kiswahili kilianza kutiliwa mkazo katika shughuli zote nchini Kenya. Kwa upande wa msimamo wa nchi lugha hii ilionekana yenye manufaa katika kuleta umoja na kuwaunganisha wananchi wote. Jambo hili ni muhimu kwa maendeleo ya nchi iwayo yote. Umoja huleta maelewano na undugu. Hali hizi mbili zinapokuwapo, amani husambaa nchini mote.

Tukitazama mfumo wa elimu wa 8-4-4, Kiswahili kimepewa nafasi sawa katika ratiba za shule kama lugha ya Kiingereza. Kiswahili kinatahiniwa kama somo muhimu kuanzia shule ya msingi hadi shule ya upili. Kinyume na enzi za zamani, siku hizi mwanafunzi anayesoma Kiswahili, hata asipofaulu vizuri katika lugha ya Kingereza ana nafasi sawa ya kupata kazi kama wengine.

**<u>Maswali</u>**

**a)** Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno 80**.** **(alama 7)**

Matayarisho

**Jibu**

**b)** Eleza vile Kiswahili hakikuthaminiwa na namna hali hii inavyobadilika. (**alama 8)**

**Matayarisho**

**Jibu**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) Toa **<u>maelezo</u>** ya jinsi ambavyo hewa huzuiliwa wakati wa kutamka sauti hizi. **(alama 2)**

**i) /p/.................................................................................................................................**

**ii) /ch/..............................................................................................................................**

**iii) /m/.....................................................................................................................**

**iv) /r/.......................................................................................................................**

(b) Tenga silabi katika neno: Alimhukumu. **(alama 1)**

(c) Tunga sentensi moja yenye kitenzi shirikishi kikamilifu na vitenzi sambamba. **(alama 3)**

(d) Tumia neno **<u>mji</u>** kama **kielezi cha mfanano**. **(alama 1)**

(e) Onyesha **namna tatu** za kutumia kiambishi “ji” katika **sentensi moja**, kisha ueleze **matumizi** husika. **(alama 3)**

(f) Ziweke nomino hizi katika **ngeli** zake. **(alama 2)**

i) waya ..........................................................................................................

ii) Kilembwe ..........................................................................................................

(g) Tambua virai vilivyopigiwa mistari ni vya **aina** gani kisha uonyeshe **miundo** yake. **(alama 4)**

**(i)** Kikapu kilichofumwa juzi kitauzwa marikiti.

**(ii)** Wenzetu walikuwa wakijinaki kabla ya dimba.

(h) Eleza **maana mbili** za sentensi**:** Zainabu alisema atakusaidia. **(alama 2)**

(i) Onyesha **majuku** ya mofimu katika neno**:** awaliaye **(alama 3)**

**(j) Andika kinyume:** Aliiangika picha ukutani baada ya sherehe. **(alama 2)**

(k) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo bila kutumia kiambishi ku. **(alama 2)**

i) Tuma ..........................................................................................................

ii) Pinda ..........................................................................................................

(l) Eleza tofauti iliyopo kati ya ukanushaji na kinyume. **(alama 2)**

(m) Andika kwa usemi wa taarifa: "Viungo hivi havitatosha kuunga mchuzi wenu", mpishi alalamika. **(alama 2)**

(n) Tumia **visanduku** kuchanganua sentensi ifuatayo**:** Alipotuona alitupuuza, lakini sisi tulimsalimia. **(alama 4)**

**(o)** Tumia vitate vya jua , toa na baka katika sentensi **tatu tofauti.** **(alama 3)**

**(p)** Kamilisha kwa viigizi mwafaka. **(alama 2)**

**(i)** Ameanguka .......................... matopeni.

**(ii)** Mlango ulibishwa ..............................

**(q)** Tofautisha sentensi. **(alama 2)**

**(i)** Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.

(ii) Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.

## 4. ISIMU JAMII (Alama 10)

**Maswali**

**a)** "........ unaweza kukata rufaa iwapo unaonelea kuwa umehiniwa ........."

**i)** Bainisha sajili ya mazungumzo haya. **(al.1)**

**ii)** Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu. **(al.4)**

**b)** Jadili changamoto zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sas**a.(al.5)**

# KCSE 2026 FINAL PREDICTIONS

## JARIBIO LA 10

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA…………………………………………………………………………………………**

**SHULE………………………………………………… SAHIHI………………………**

**NAMBARI YA USAJILI…………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**FASIHI**

**MAAGIZO**

***a)*** *Jibu maswali manne pekee.*

***b)*** *Swali la kwanza ni la lazima.*

***c)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Hadithi fupi, Ushairi, Tamthilia na Fasihi Simulizi.*

***d)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

***e)*** *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

***f)*** *Majibu yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**SEHEMU YA A: NGUU ZA JADI** **(ALAMA 20)**

**1. SWALI LA LAZIMA**

"Ndugu zangu, ukabila ni sumu ya nyoka. Ukabila huangamiza maendeleo ya nchi hata kama imestawi kiasi gani."

- Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(alama 4)**
- Eleza umuhimu nne wa msemaji wa kauli hii. **(alama 4)**
- Onyesha mbili za uandishi zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama 2)**
- Kwa kutumia hoja zisizopungua kumi, jadili maudhui ya ukabila yanavyojitokeza katika riwaya hii. **(alama 10)**

**SEHEMU YA B: BEMBEA YA MAISHA**

**JIBU SWALI LA 2 AU LA 3**

**2**. Wanasema kuwa Mungu hamtupi mja wake. Kweli iliyoje!

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Fafanua sifa za msemaji. **(alama 4)**

(c) (i) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. **(alama 6)**

(ii) "Lakini inakujuzu uelewe kuwa dunia ni nyumba ya mtihani." Onyesha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya *Bembea ya Maisha*. **(alama 6)**

**AU**

**3**. (a) ***Changanua mbinu za kimtindo katika dondoo lifuatalo***. **(alama 8)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (Kimya). Siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (Kimya). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (Kimya). **Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya**. Maisha mapya. Pombe! (kama anayesemea pombe). Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu.

(b) Kauli iliyokolezwa wino katika dondoo inadokeza nia ya kubadilika kwa mzungumzaji. Kwa kurejelea tamthilia nzima, onyesha jinsi mwandishi alivyoshughulikia suala la mabadiliko. **(alama 12)**

**SEHEMU YA C: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO ;IBU SWALI LA 4 AU LA 5**

**4. MSIBA WA KUJITAKIA** **(ALAMA 20)**

"Tayari alikuwa amefanya kosa. Kosa ambalo alifahamu lilikuwa la kujitakia."

- Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
- Bainisha toni inayodokezwa na dondoo hili. **(alama 2)**
- Hadithi ya *Msiba wa Kujitakia* ina matukio mengi yanayoonyesha kinaya. Thibitisha.**(ala 6)**

d)“Tamaa mbele mauti nyuma.” Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi: Nilitamani. **(alama 8)**

**AU**

**5.** Jadili jinsi maudhui ya **usaliti** yanavyojitokeza katika hadithi zifuatazo: **(alama 20)**

- Toba ya Kalia
- Kifo cha Suluhu

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

**6. SHAIRI HURU** **(ALAMA 20)**

***Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali***

Nimeyaandika maneno haya Kwa
niaba ya:
Mamilioni wasio malazi
Wabebao vifurushi vilivyo wazi Wazungukao
barabarani bila mavazi ... milki yao ya Maisha.
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki Wiki
baada ya wiki
leo sumu au spaki
leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya: Vijana walio
mitaani wale mayatima wa
maskini wazungukao mapipani
kila pembe mjini kuokota sumu
kutia tumboni
kujiua bila kujua ili
kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza walao
chakula kilichooza wachukuao
choo wakijipakaza polepole
wakijiangamiza katika vyumba
vyao
baridi na giza kwa sababu hawana
watazama wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu Kwa sababu ya
madawa tifutifu yatiwayo vyakulani
yakitufanya wafu bila ya mtu kuona
kama kwamba sote tu vipofu,

Na kwa niaba yete sote;
Tuliofungwa vifungoni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni, machoni
Tuliotiliwa sumu, malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini ili 'maendeleo'
yaendelee kwenda njiani huku yakitema
machicha ya roho zetu.

**Maswali**

**a)** Hili ni shairi la aina gani? Tetea jibu lako. **(alama 2)**

**b)** Bainisha toni ya shairi hili . **(alama 2)**

**c)** Tambua aina tatu za urudiaji zinazojitokeza katika shairi. **(alama 3)**

**d)** Huku ukitoa mifano eleza namna mtunzi alivyotimiza arudhi za kishairi. **(alama 3)**

**e)** Eleza matumizi ya.

i) Mistari mishata **(alama 1)**

ii) Mistari kifu **(alama 1)**

f) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. **(alama 2)**

g) Tambua aina za taswira katika shairi hili. **(alama 2)**

h) Mshairi anazungumza kwa niaba ya watu mbalimbali. Jadili.: **(alama 4)**

**AU**

**7. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali.***

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyahutubu
Wayasome ndugu zangu, wa mbali na karibu Cha
wenye raha na taabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, chenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu Kuta
na kucha twahanja, kutafuta matulubu Cha wenye
raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa *balaa*, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu Na
machache ya kufaa, ila mengi ya udubu Cha
wenye raha na tabu ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina, Saidi Ali Rajabu
Wengune kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu Cha
wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu Cha
wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu Maneno
ya kiujuvi, hujipaka hata shabu Cha wenye raha na
tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenye dini, watiio Wahabu
Mashekhe misikitini, humo hufanya muhibu
Mapadri kanisani, huvihubiri vitabu Cha wenye
raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa, na moyo *kisebusebu*
Tunakaribia kufa, kwa kushindwa kujimudu Cha
wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Na mengine sitotaja, msinambe nina gubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

**Maswali**

- Eleza mambo yanayojitokeza katika shairi hili. **(alama 3)**
- Ainisha bahari katika shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. **(alama 3)**
  - Mpango wa maneno
  - Vipande
  - Vina

- Onyesha jinsi mbinu alizotumia mshairi kukidhi mahitaji ya kiarudhi. **(alama 3)**
- Onyesha umbo la ubeti wa 3. **(alama 3)**
- Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi **(alama 4)**
- Mshairi huyu ni bingwa kwa kutumia lugha. Thibitisha. **(alama 2)**
- Fafanua toni katika shairi hili. **(alama 1)**
- Eleza maana ya neno ***kisebusebu*** kama lilivyotumiwa katika shairi **(alama 1)**

**8. <u>SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI</u>** **(ALAMA 20)**

Mtoto wetu lala
Mtoto wetu lala
Mama ameenda sokoni
Kununua ndizi, atakuja na ndizi nyingi
Ndizi kubwa itakuwa yako
Utakula yote mtoto wetu
Kwa sababu mama anakupenda
Mama anakupenda
Mtoto wetu lala
Baba ameenda shambani kuvuna
Mimi mlezi wako nitakutunza kwa upendo
Nitakuandalia samaki kama jana
Mtoto wetu lala
Mama anakupenda sana.

**<u>Maswali</u>**

- Huu ni wimbo wa aina gani. Thibitisha. **(alama 2)**
- Taja na uthibitishe shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii asili ya wimbo huu. **(alama 2)**
- Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anaimbia nani? **(alama 2)**
- Eleza mbinu ambazo mwasilishaji wa utanzu huu anaweza kutumia ili kufanikisha uwasilishaji wake. **(alama 2)**
- Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii. **(alama 5)**

**f)** Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii **(alama 2)**

**g)** Umepewa wajibu wa kutafiti mbolezi katika jamii yako. Pendekeza mbinu ambazo ungetumia kutafiti kipera hiki. **(alama 5)**

# To Obtain Copies of Respective Marking Schemes / Answers

## CALL/TEXT/WHATSAPP

## 0746-222-000
## 0753-222-000

kcsepredictions@gmail.com

*This is a Copyright Property of Mwalimu Consultancy Ltd.*

## Powered By Mr Isaboke

# SUCCESS

## POLITE NOTE TO 2026 KCSE CANDIDATES

***In the event that any of these revision questions closely match or appear in the upcoming national examinations, please stay composed.***

***Do not panic, and approach your papers with confidence.***

***BEST OF LUCK IN YOUR EXAMS!***

***REGARDS***

***MWALIMU CONSULTANTS – PANEL OF KNEC EXAMINERS***